

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA SABA**

**Kikao cha Kwanza – Tarehe 4 Aprili, 2017**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**WIMBO WA TAIFA**

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge Waliimba Wimbo wa Taifa)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Natoa nafasi kwa Waheshimiwa Wabunge mnaoingia, naomba mfanye haraka kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, nawakaribisha kwenye Mkutano wa Saba, Kikao cha Kwanza, Katibu! *(Vigelegele)*

**DKT. THOMAS KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:**

**KIAPO CHA UAMINIFU**

Mheshimiwa Mbunge afuatae aliapa Kiapo cha Uaminifu:-

Mhe. Salma Rashid Kikwete. *(Vigelegele/Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nashukuru kwa makofi yenu. Tuendelee sasa maana nilikuwa nasubiri kidogo nione mama anakaa wapi ili akisimama kwenye maswali

nijue yupo wapi maana leo nataka nimpe swali la kwanza.  
Katibu tuendelee! (*Makofi/Kicheko/Vigelegele*)

**DKT. THOMAS KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:**

**TAARIFA YA SPIKA**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, katika Mkutano wa Sita wa Bunge, Bunge lllipitisha Miswada ya Sheria ya Serikali miwili ifuatayo:-

(i) Muswada wa Sheria ya Huduma ya Msaada wa Kisheria (*The Legal Aid Bill, 2016*); na

(ii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.4 wa Mwaka 2016 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendment) No. 4 Bill 2016*)

Kwa Taarifa hii, npenda kuliarifu Bunge hili Tukufu kwamba tayari Miswada hiyo miwili imepata kibali cha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwa sheria za nchi zinazoitwa:-

(i) Sheria ya Huduma ya Msaada wa Kisheria Na.1 ya Mwaka 2017 (*The Legal Aid Act No.1, 2017*); na

(ii) Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.4 ya Mwaka 2017 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendment) No.4, Act No.2 2017*).

Mwisho wa Taarifa ya Spika, Katibu! (*Makofi*)

**DKT. THOMAS KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na maswali, naomba nichukue fursa hii kuwatambulisha wageni maalum waliopo katika *gallery* ya Spika. Mgeni wetu

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

wa siku ya leo sio mwingine bali ni Mheshimiwa Rais Mstaafu Mheshimiwa Jakaya Kikwete.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walipiga makofi na vigelegele kwa muda)*

**SPIKA:** Kwa makofi hayo, sasa naomba mumppe *standing ovation*. Mpigieni makofi mkiwa mmesimama.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walisimama wakiendelea kupiga makofi na vigelegele)*

**MBUNGE FULANI:** Tumeku-*miss*, tumeku--*miss!*

**WABUNGE FULANI:** Rais, Rais, Rais.

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MBUNGE FULANI:** Tunakukumbuka.

**SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge...

**MBUNGE FULANI:** Urudi.

**SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge.

**MBUNGE FULANI:** Tunaomba arudi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane...

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Msigwa hujapiga makofi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane nawaomba sana.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge waliendelea kupiga makofi na vigelegele)*

**MBUNGE FULANI:** Tunaomba arudi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, binafsi mimi ni kipindi cha nne humu Bungeni, sijawahi kuona mgeni amepokelewa kwa kiwango hiki.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walipiga makofi na vigelegele kwa muda)*

**MBUNGE FULENI:** Aje atusalimie.

**MBUNGE FULANI:** Tunakukumbuka.

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa tuendeleo.

**MBUNGE FULANI:** Aje atusalimie chini hapa.

**SPIKA:** Naomba tuendeleo kwa jambo moja. Naomba tusikilizane maana yake...

**MBUNGE FULANI:** Aje atusalimie ndani.

**MBUNGE FULANI:** Ajeeee.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge waliendelea kupiga makofi na vigelegele kwa muda)*

**MBUNGE FULANI:** Toa hoja.

**MBUNGE FULANI:** Tengua kanuni.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, inaelekea hata waliom-miss nao wapo! *(Kicheko/Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Wapooo. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Pamoja naye, amefuatana na mwanae Ndugu yetu Ally Kikwete. Karibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais Mstaafu, tunakushukuru sana kuwa pamoja nasi asubuhi ya leo. *(Makofi/Vigelegele)*

Tunaendelea na maswali. Swali la kwanza linaenda Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora) na litaulizwa na Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, Mbunge wa Mtambwe.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na furaha walionayo Waheshimiwa Wabunge, naomba swali langu namba moja lipatiwe majibu. *(Makofi)*

Na. 1

### **Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) Awamu ya Tatu**

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA** aliuliza:-

Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) upo katika Awamu ya Tatu ya utekelezaji wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini ili ziweze kumudu mahitaji ya chakula, elimu, afya na lische bora kwa watoto:-

(a) Je, Serikali haioni ipo haja ya kuongeza viwango vya ulipaji kwa kaya maskini hasa ukizingatia upandaji wa bei za mahitaji ya kila siku na kuporomoka kwa thamani ya sarafu yetu?

(b) Je, ni vigezo gani vya uhakika vinatumika ili kupata kaya maskini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa, Mbunge wa Jimbo la Mtambwe, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini ni wa miaka kumi na utatekelezwa kwa vipindi viwili vya miaka mitano mitano kuanzia mwaka 2013 – 2023. Madhumuni ya Mpango huu ni kuwezesha kaya maskini kuongeza kipato na fursa na kuinua kiwango cha matumizi yao.

Mheshimiwa Spika, kiwango kinachotolewa kwa walengwa ni ruzuku ambayo ni kichocheo cha kuifanya kaya iweze kujikimu hasa katika kupata mahitaji muhimu huku ikiendelea kujiimarisha kiuchumi kwa kuweka akiba na kutekeleza miradi ya ujasiriamali ili iweze kusimama yenyewe na kujitegemea baada ya kutoka kwenye umaskini uliokithiri.

Mheshimiwa Spika, ruzuku inayotolewa kwa walengwa imeongezwa baada ya kufanyiwa mapitio kwa kuangalia hali halisi. Hata hivyo, ieleweke kwamba viwango vinavyotolewa vilipangwa hivyo ili kaya maskini iendeleo kujishughulisha na kazi nyingine za kuongeza kipato na isitegemee ruzuku peke yake. Kwa uzoefu uliopatikana, umeonesha kwamba kwa kiwango hicho walengwa wameweza kuboresha maisha yao kwa kufanya shughuli mbalimbali ikiwemo kilimo, ufugaji, ujasiriamali na ujenzi wa nyumba bora, hivyo viwango hivyo vya ruzuku sio kidogo kama wengi wetu tunavyodhani.

(b) Mheshimiwa Spika, vigezo vya kupata kaya maskini huainishwa na jamii katika mkutano wa hadhara unaoendeshwa na wawezeshaji kutoka Halmashauri za Wilaya na kusimamiwa na viongozi wa vijiji/mitaa/shehia. Jamii huweka vigezo vya kaya maskini sana katika maeneo yao. Hata hivyo, vigezo vikuu katika maeneo mengi ni kaya kukosa/kushindwa kugharamia mlo mmoja kwa siku, kaya kuwa na watoto ambao hawapati huduma za msingi kama elimu na afya kutokana na kuishi katika hali duni, wazee, wagonjwa wa muda mrefu na watoto yatima wanaoishi katika mazingira magumu na pia kukosa makazi ya kudumu au nyumba na mavazi muhimu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Khalifa, swali la nyongeza.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, kwanza mimi na-*declare my interest* kwamba ni Mjumbe wa Kamati yako ya Kudumu ya Utawala na TAMISEMI. Kwa hivyo, katika ziara zetu mbalimbali tumepata ushuhuda wa wanufaika wa kaya maskini na kiwango fulani wamenufaika kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na kunufaika kwao bado haijaondoa umuhimu wa kuweza kuongezewa hii ruzuku kwa sababu kama nilivyosema katika swali langu la msingi kila siku maisha yanapanda, shilingi yetu inaporomoka na bei ya bidhaa inaongezeka. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri anaonaje basi wakaweza kupewa viwango hivi wanavyopewa kwa mkupuo walau wa miezi sita ili ile tija ya kuweza kuendesha biashara zao, kujenga makazi yao ikapatikana?

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili dogo, mimi nashukuru katika Jimbo langu pia mradi huu katika baadhi ya shehia unaendelea lakini kuna usumbufu wale walengwa kutoka katika vijiji vingi wanakusanyika katika *center* moja. Waziri anaonaje akaongeza vituo vya kulipia ili wale watu ambao wamekusudiwa kupewa ruzuku hii wasipate matatizo hasa ukizingatia wengine ni wanyonge sana, wengine ni watu wazima mno...

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Khalifa ahsante kwa swali lako. Majibu Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mheshimiwa Angellah Kairuki.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, nimeeleza katika majibu ya swali langu la msingi. Kwanza kabisa, ukiangalia mradi huu, kabla hatujaanza uhawilishaji mwaka 2013 tulianza mpango wa majaribio mwaka 2008 kwa miaka mitano katika Halmashauri tatu za Chamwino, Bagamoyo pamoja na Kibaha. Katika mpango huo wa majaribio, kaya 26,000 zilishiriki katika mpango huu.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia mwanzoni wakati programu inaanza, wakati huo wa majaribio, kiwango cha juu kabisa kilikuwa ni Sh.17,500/=. Hata hivyo, tulipoanza mpango tulipandisha mpaka Sh.34,000/= na ilikuwa haiangalii watoto walioko katika kaya, haingalii watoto wanaopata huduma za kiafya na zinginezo. Nipende tu kumwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba tumeongeza, kwa sasa hivi kiwango cha juu kabisa ni Sh.76,000/= vilevile wanapata fursa pia ya kupata ujira, kwa siku 60 kila mwaka wanapata takribani Sh.138,000 kwa Sh.2,300 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda kusema kwamba katika majaribio ilionekana ukiwapa kiwango kikubwa sana inawezekana wakabweteka na wasiweze kufanya shughuli zingine za ujasiriamali na wakajitegemea tu kupitia ruzuku hii. Kwa hiyo, ilionekana kwa kweli kiwango hiki kinafaa na tumefanya majaribio na wako wengi ambao wameweza kunufaika na kupata maendeleo katika maisha yao.

Mheshimiwa Spika, katika swali lingine kwamba wapewe sasa kwa mkupuo wa miezi sita, hoja yake Mheshimiwa tunaiona, napenda tu kusema kwamba tunaendelea kuifanyia kazi ili kuona kama inawezekana miezi sita au miezi mitatu na nini kinaweza kikafanyika. Kwa sasa nisiseme kama tumekubali, lakini niseme tunaona hoja ni ya msingi tuichukue twende tukaifanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na hoja ya kuongeza vituo vya kulipia fedha na yenyewe pia niseme tunaichukua ili kuona ni kwa namna gani tunaweza tukawarahisishia na kuwasogezea huduma karibu zaidi walengwa wetu.



**SPIKA:** Ahsante. Sasa hapa, mbona mko wengi hivyo, nitaanza pale nyuma CCM, Mheshimiwa Mchungaji na ACT, maswali matatu hayo, tuendelee.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kila Halmashauri ya Wilaya ina Mratibu wa *TASAF* na waratibu ndiyo wameandikisha kaya maskini, walijua kabisa kwamba kaya hii ni maskini. Hivi karibuni kuna kaya ambazo zimeondolewa kwamba hazina sifa na wanaambiwa warejeshe fedha, wengine ni wazee kabisa. Mheshimiwa Waziri nani mwenye makosa, ni mratibu aliyeorodhesha au ni yule ambaye ameambiwa kwamba alipe hizo fedha? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo muhimu sana, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mheshimiwa Angellah Kairuki.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze kwa namna ambavyo amekuwa akifuatilia utekelezaji mzima wa mpango huu, lakini zaidi namna ambavyo amekuwa akifuatilia kaya zile ambazo zimeondolewa. Mpaka sasa tumeshaondoa kaya 63,819 katika maeneo 162 ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda tu kusema kwamba, wale ambao wamelengwa kuondolewa katika uhakiki huu ni zile kaya ambazo hazikustahili kuingizwa katika mpango. Tumekuwa tukishuhudia pia katika zoezi hili, kama mnavyotambua wakati wa utambuzi na uandikishaji, chombo kikuu kinachoshiriki ni mkutano wetu mkuu wa kijiji au katika shehia lakini unakuta wengine waliwaingiza wenye uwezo matokeo yake baadaye wanajikuta wanakuja kuondolewa tunakuja tunasikia maneno kama hayo.

Mheshimiwa Spika, nipende tu kusema kwamba, kama kweli kaya ilikuwa ni maskini, ikawa imejiboreshea maisha haikutakiwa kuondolewa bila kufuata vigezo vya msingi. Tumeanza kufanya zoezi hili, tumeshawaandikia

Wakurugenzi wote tangu mwezi Februari waweze kupitia kwa kina. Napenda tu kusema kwamba waratibu wengi pia walishiriki, hawakuwa makini katika ufuatiliaji na katika tathmini zao na ndiyo maana tayari tumeshawachukulia hatua waratibu zaidi ya 91 na tutaendelea kufanya hivyo kila ikibidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda tu kusema kwamba, wale ambao tunawalenga ni wafanyabiashara, unakuta kuna mtu alikuwa ana bucha na mambo mengine ameingizwa, haiwezekani! Vilevile unakuta wengine ni watumishi wa umma wameingizwa katika mpango hawastahili kuanzia siku ya kwanza, hao ndio ambao tunawalenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda tu kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa namna ambavyo wamekuwa wakifuatilia suala hili. Tutaendelea kuwafuatilia na tutaendelea kuchukua hatua. Kwa wale ambao ni maskini kweli kwanza wanatakiwa warudi kwenye mpango na si kumfuatilia aweze kurudisha fedha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, swali fupi la nyongeza.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, toka mpango huu umeanza baadhi yetu tuli-*challenge* sana kwamba haukuanza kubadilisha fikra za watu kabla ya kuwapa hela. Nataka nimuulize Waziri ni kwa kiwango gani anaweza akaliambia Bunge hili huu mpango wa kugawa hizi fedha umeleta *impact* katika jamii, kwa sababu bado hali ya umaskini imeendelea kuwa kubwa katika Taifa letu.

**SPIKA:** Swali lake liko juu juu sana lakini Mheshimiwa Waziri kama una majibu, tafadhali Mheshimiwa Kairuki.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Spika,

naamini, bahati nzuri wiki iliyopita tu tulikuwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, tulikuwa liringa Mjini, tumetembelea walengwa wale na kaya zake. Sasa kama leo anasema kaya zile kweli hazijanufaika na hazijaondoka kwenye umaskini, kwa kweli inabidi hata wapiga kura wamwangelie kwa macho mawili, mawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ukiangalia tumefanya tathmini kuangalia ni kwa namna gani fedha hizi zimeweza kuchochea mabadiliko. Vilevile ukiangalia katika *TASAF* Awamu ya I na II, kulikuwa hakuna ruzuku ya uhawilishaji lakini ilikuja kuonekana katika Watanzania asilimia 28.3 wenye pengo la umaskini walikuwa hawawezi kumudu gharama za kupeleka familia zao katika matibabu, wengine watoto wao walikuwa wamedumaa, wengine walikuwa hawapati lische ya kutosha, wengine walikuwa hata shuleni mahudhurio hawahudhuri vizuri. Ukiangalia sasa hata liringa peke yake zaidi ya asilimia 70 mpaka 90 mahudhurio yameimarika, wengine sasa zaidi ya asilimia 10 mpaka 15 wanaanza kukaribia kuondoka katika pengo la umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nipende tu kusema wengi wameboresha mavazi, wengi wameboresha makazi yao, wengi sasa ukiangalia hata kwa zile kaya zilizokuwa zinajiweza ambazo zilikuwa haziwezi kuwavalisha watoto wao shuleni, wanaangalia kama mtoto maskini anaweza kuvaa nadhifu basi na yeye kidogo anajiongeza. Kwa hiyo, kwa kweli ni Mfuko ambao umekuwa na manufaa sana na nimwombe Mheshimiwa Msigwa aendelee kufuatilia kaya zake na aendelee kuziunga mkono. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Zitto Kabwe swali la mwisho la nyongeza.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa ya umaskini Tanzania ni kwamba idadi kubwa ya watu ama wako chini kidogo ya mstari wa umaskini au juu kidogo ya mstari wa umaskini. Kwa hiyo, hata

wakipata fedha hizi za *TASAF* wakipata *shock* yoyote ya kimaisha wanarudi chini kwenye mstari wa umaskini na wanakuwa maskini, kwa hiyo, juhudi zote hizi zinakuwa hazijaleta manufaa yanayotakiwa. Serikali haioni kwamba umefikia wakati muafaka katika fedha hizi za *TASAF* kuwe na *component* ya *social protection* ili kuhakikisha kwamba baadhi ya watu hawa wanaingizwa kwenye hifadhi ya jamii, wanaweza akiba, wanaweza kupata mikopo midogo midogo ya kuendesha biashara zao, wanaweza wakapata bima ya afya, ili watakapopata *shock* wasirudi tena kwenye mstari wa umaskini? Haoni kuna haja ya kufanya hivyo sasa hivi kwenye *TASAF* inayoendelea? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, (Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora), Mheshimiwa Angellah Kairuki tafadhali!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru maana ni hoja ambayo amekuwa akiifuatilia mara kwa mara. Tulipofanya semina katika Bunge hili ambayo iliendeshwa na *TASAF* pia aliweza kuhoji swali kama hili.

Mheshimiwa Spika, napenda tu kusema kwamba, lengo la *conditional cash transfers* kokote duniani ni kuhakikisha kwamba mwisho wa siku ni kuwa na *social protection* moja ambayo inaunganisha kuanzia mwanzo mpaka mwisho. Sisi kama *TASAF* tumeanza na sasa watoto wenye miaka sifuri mpaka tano, mpaka sasa hivi watu wazima walau kuna hizo *component* tatu kwenye miradi ya ujira, tunatoa pia ajira za muda, tunatoa miradi ya miundombinu, tuna *targeted infrastructure* pamoja na mingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kusema, tunaiona hoja yake lakini kwa sasa ngoja tumalizie awamu ya kwanza ya awamu ya tatu. Tutakapokuja kusanifu sasa awamu ya pili itakayoanza mwaka 2019/2020 tutaweza kuona ni kwa namna gani swala hili linaweza kuzingatiwa.

**SPIKA:** Tunaendelea na swali linalofuata Waheshimiwa Wabunge, swali namba mbili.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika...

**SPIKA:** Aah! Mheshimiwa Salma Kikwete tafadhali swali la nyongeza. *(Makofi)*

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza, lakini kabla ya kuuliza swali la nyongeza, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu na nimshukuru Mheshimiwa Rais wangu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuiteua kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la nyongeza ni kuhusu huduma ya *TASAF*. Serikali ina mpango gani mahsusi wa kuongeza huduma hii hasa kwa watu wetu maskini kutoka katika Mkoa wetu wa Lindi? *(Makofi/Vigelegele)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Majibu kwa swali hilo muhimu Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze kwa namna ambavyo amekuwa akifuatilia maendeleo ya jamii, lakini zaidi kwa siku ya kwanza tu ameweza kuuliza swali hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika Mkoa wa Lindi nikitolea tu mfano kwa sasa tuko Lindi *DC*, Lindi Manispaa, Nachingwea, Ruangwa pamoja na maeneo mengine. Niseme tu kwamba tumepokea hoja hii, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sasa tumefikia asilimia 70 tumebakiza asilimia 30 yenye vijiji 5,690 na tumepanga katika mwaka huu wa fedha unaokuja wa 2017/2018 tutaweza kutambua na kuandikisha kaya zilizobakia 355,000 na naamini Lindi pia itakuwa ni mojawapo.

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaenda Wizara ya Maliasili na Utalii, swali linaulizwa na Mheshimiwa Amina Saleh Mollel!

Na. 2

### **Marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro**

**MHE. AMINA S. MOLLEL** aliuliza:-

Wakazi wanaoishi katika eneo la Hifadhi ya Ngorongoro wamekatazwa kulima kwenye maeneo wanayoishi kwa mujibu wa sheria hali iliyochangia wakazi wengi katika eneo hilo ambao ni wafugaji kukabiliwa na njaa pamoja na umaskini mkubwa wa kipato:-

Je, ni lini Serikali itarekebisha Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi (Ngorongoro *Conservation Area Act*), 1959 Revised Edition, 2002) ili wananchi wa maeneo haya wapate maeneo kwa ajili ya shughuli zao za kilimo na ufugaji?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Saleh Mollel, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kwa mujibu wa sheria iliyoanzisha Hifadhi ya Ngorongoro, Sheria ya Kuhifadhi Eneo la Ngorongoro ya mwaka 1959 iliyopitiwa mwaka 2002 (*The Ngorongoro Conservation Area Act 1959, R.E 2002*) wananchi wakaazi katika eneo la Hifadhi ya Ngorongoro hawaruhusiwi kulima bali kufuga peke yake.

Mheshimiwa Spika, kutokana na zuio la kisheria la kulima, wakazi wa eneo la Ngorongoro ambao kwa asili yao ni wafugaji, wamekuwa wakitengewa bajeti ya kununulia mahindi ambapo takribani tani 3,600 hugawiwa bila malipo kila mwaka kwa matumizi ya chakula hususan kwa wale

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

wenye kipato cha chini na wasiojiweza. Kwa wale wenye uwezo, mahindi hayo huuzwa kwao kwa bei pungufu ya bei ya soko.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto ya chakula, mnamo mwaka 2007, mamlaka ilianza mchakato wa kupata maeneo ya kilimo nje ya hifadhi kwa kutenga bajeti na kuwezesha mradi wa JEMA. Malengo mawili ya mradi wa JEMA ulioko katika Kata ya Oldonyosambu ni haya yafuatayo:-

(a) Kuwaondoa wahamiaji walioingia ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro ambao hawakuwa wakazi halali kwa kuzingatia kwamba wakazi halali ni wale waliokuwepo pamoja na uzao wao wakati eneo la Hifadhi ya Ngorongoro lilipotangazwa rasmi mwaka 1959.

(b) Kutoa fursa kwa wakazi wenyeji na halali ambao wangependa kufanya shughuli za kilimo na ufugaji nje ya hifadhi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mradi huu kuendelea, tathmini ya awali inaonesha upungufu kwa baadhi ya waliohamishiwa eneo la mradi kuuza maeneo waliyopewa na kurejea kinyemela ndani ya hifadhi. Kutokana na upungufu huo, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kwa kushirikiana na uongozi wa Wilaya ya Ngorongoro, inaendelea kuchukua hatua ya kuzuia uuzwaji wa maeneo katika eneo la mradi. Aidha, kwa kuwa maeneo yaliyopatikana hapo awali hayakuweza kutosheleza mahitaji, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kwa kushirikiana na wadau wengine inaendelea kutafuta maeneo mengine yatakayotumika kwa kilimo.

Mheshimiwa Spika, sheria iliyoanzisha eneo la Hifadhi ya Ngorongoro ilianza kutumika zaidi ya miaka 50 iliyopita na Serikali iko kwenye maandalizi ya awali ya kufanya marekebisho yake. Ni muhimu kuzingatia kwamba, katika marekebisho hayo Serikali itaweka msisitizo zaidi katika kuboresha shughuli za uhifadhi wa eneo la Ngorongoro ili libakie katika orodha ya maeneo ya urithi wa dunia.

**SPIKA:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Amina Mollel.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na nashukuru pia kwa majibu kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa majibu ya Mheshimiwa Waziri ni kwamba Serikali iko mbioni kufanya marekebisho ya sheria hii. Napenda kufahamu ni lini sasa Serikali itafanya marekebisho haya na kutenga eneo mahsusi kwa ajili ya wakazi wanaoishi katika eneo hili la Bonde la Ngorongoro ili waweze kujihusisha na kilimo kwa sababu sio mazao yote yanayoharibu mazingira?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, kwa kuwa ukosefu wa maji kwa mifugo hususan msongamano ndani ya eneo dogo na kuharibu mazingira na kwa kuwa hifadhi hii bado ina maeneo ambayo yanaweza kutengwa kwa ajili ya mifugo iweze kupata maji na Mheshimiwa Waziri Mkuu alishaigiza Wizara hii kuhakikisha kwamba inatenga maeneo hayo ili wafugaji waweze kupata maeneo hayo kwa ajili ya kunyweshea mifugo yao. Je, ni lini Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro itaweka maeneo haya maji na wananchi wanaoishi katika Bonde hili la Hifadhi ya Ngorongoro waweze kunywesha mifugo yao katika maeneo hayo na siyo kwenda kuharibu mazingira kama ambavyo sasa wanavyodaiwa kufanya?

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Amina Mollel. Majibu ya maswali hayo, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Injini Ramo Makani.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, katika swali lake la kwanza anataka kujua ni lini mabadiliko ya sheria kama ambavyo tumejibu katika swali la msingi yanafanyika? Mchakato wa mabadiliko ya sheria unatangiwa na shughuli kadhaa za kitaalam ambapo kutokana na shughuli hizo za kitaalam ndipo mapendekezo ya mabadiliko ya sheria yanapelekwa katika hatua



mbalimbali za Serikali ili hatimaye mabadiliko ya sheria yale yaweze kuwa na tija kwa sababu yatakuwa yana-*input* ya kitalaam.

Mheshimiwa Spika, hivi ninavyozungumza, katika kipindi cha wiki moja kikosi maalum cha watu wanaotakiwa kufanya sensa kama jambo la kwanza kabisa la kulfanya ili kujua ukweli wa hali halisi ya Ngorongoro kitaanza kazi. Kazi ambayo itafanyika kwa muda wiki moja. Hii inatokana na ukweli kwamba mwaka 1959 wakati Ngorongoro inatengwa kama eneo la hifadhi kulikuwa na jumla ya wakazi 8000 ndani ya eneo lile. Kufikia mwaka 2013 tayari kulikuwa na wakazi jumla ya 87,851, hii ni takribani wastani wa ongezeko la wakazi 1500 kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, changamoto hii ni kubwa na hivyo hata mabadiliko ya sheria yanatakiwa yaangalie uhalisia ambao utakuwa ni uhalisia wa kisayansi. Kwa hiyo, nimuahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, ndani ya kipindi cha mwaka wa fedha ujao tutakuwa tumeanza na kukamilisha utaratibu wa mabadiliko ya sheria inayohusika.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili anazungumzia juu ya suala la ukosefu wa maji na ambalo lina maagizo mahsusi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ni kweli, kulikuwa na maagizo ambayo yalikuwa yanataka kutatua changamoto ya maji katika kipindi cha mpito wakati ambapo tunasubiri mabadiliko yale ya sheria ambayo yataweka misingi ambayo itakuwa ni ya kudumu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mpito suala la maji kwa ajili ya mifugo linashughulikiwa kwa kujenga mabwawa katika maeneo ambayo yanaonekana kwamba uwepo wa mabwawa katika maeneo hayo utatatua changamoto ya mahitaji ya maji kwa mifugo. Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro imetenga fedha katika bajeti hii na Waheshimiwa Wabunge mkiipitisha, basi tunaweza kutatua tatizo hili kwa namna ambayo itakuwa ni toshelezi. Kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Mbunge afanye subira, asubiri Bajeti

ya Serikali, bajeti ya Wizara hii itakapopita, hasa kwa upande ule wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro tutakuwa tumeweza kuweka tengeo la kuweza kutekeleza agizo la Mheshimiwa Waziri Mkuu ipasavyo.

**SPIKA:** Maswali madogo mawili ya nyongeza, Mheshimiwa Nkamia nilikuona na Mheshimiwa Cecilia Paresso.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali moja tu la nyongeza. Tatizo la Hifadhi ya Ngorongoro linafanana sana na lile tatizo la Hifadhi ya Swagaswaga ambalo linaunganisha Wilaya za Kondoza na Chemba. Kumekuwa na matatizo watu wengi wamezuiwa kulima na nilishakwenda mimi na Mheshimiwa Naibu Waziri katika eneo hilo na akatoa maagizo kwamba, ufanyike utaratibu wa kuweka mipaka upya, lakini jambo hili halijafanyika hadi sasa. Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kuweka mipaka ili wananchi wa Lahoda, Kisande, Iyoli pamoja na Handa waweze kuondokana na tatizo hili?

**SPIKA:** Majibu kwa kifupi kwa swali hilo la Kondoza, Mheshimiwa Injinia Ramo Makani.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa fursa hii. Ni kweli nilifanya ziara katika eneo hili ambalo linahusika na hifadhi yetu ya Swagaswaga na niliambata na Mheshimiwa Mbunge na ni kweli niliacha maagizo kama anavyosema. Pia siyo tu agizo, tuliendelea na utaratibu ule wa kuunda kikosi kazi ambacho kilihusisha Wizara nne na ambacho kimekuwa kikiendelea na kazi yake kwa muda wa miezi michache iliyopita. Sasa hivi kamati ile imeshaandaa mapendekezo ya awali ambayo yamekabidhiwa tayari kwa Kamati ya Makatibu Wakuu, baada ya pale yanaenda kukabidhiwa kwa Baraza la Mawaziri, baadaye kwenye ngazi za juu, ili tuweze kupata mwelekeo zaidi wa kwamba nini kifanyike ili kuweza kukamilisha utaratibu wa kuweka mipaka.

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwa maana ya maeneo yale ambayo hayana migogoro kabisa, suala la uwekaji wa mipaka limekuwa likiendelea na hifadhi kadhaa tayari zimeshakamilisha utaratibu huo. Mheshimiwa Mbunge akiniona baada ya hapa tutaweza kuangalia kwenye orodha kama eneo lake limepangiwa lini kukamilisha utaratibu wa kuweza kuweka mipaka.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Swali la mwisho Mheshimiwa Cecilia Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Wananchi wa Tarafa ya Ngorongoro wamekuwa wakikumbwa na changamoto kubwa sana kwa sababu wanaishi katika eneo la hifadhi. Hata hivyo kumekuwa na ahadi nyingi za Serikali za kumaliza hiyo changamoto lakini hakuna mafanikio na mpaka leo wananchi wale wanaishi tu kwa matumaini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba wamekataza mifugo isiingie *crater* lakini kuna changamoto ya upatikanaji wa maji. Kumeshawahi kutengwa takribani shilingi bilioni tano na zimetumika, wamejenga ranchi kwa ajili ya kuhifadhi mifugo isiingie *crater* na haitumiki. Je, ni kwa nini ranchi imejengwa kwa gharama kubwa halafu haitumiki mpaka sasa?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Injini Ramo Makani.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, changamoto za Hifadhi ya Ngorongoro ni kubwa na nyingi. Hata hivyo, napenda ieleweke kwamba katika kusimamia uhifadhi ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro jambo hili sisi wote kwa pamoja tunatakiwa tuzingatie ukweli kwamba maslahi ya mtu mmoja mmoja yatazingatiwa, maslahi ya makundi yatazingatiwa lakini mwisho wa siku maslahi ya Taifa yanayotokana na kuhifadhi eneo lile ndiyo yatakayopewa kipaumbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni kweli, hapa na pale katika kipindi chote cha uwepo wa sheria hii tunayoizungumzia ya mwaka 1959 mengi yametokea. Yako yale ambayo Serikali ilisema itatekeleza, tumetekeleza kikamilifu, yako yale ambayo bado Serikali inaendelea kuyatekeleza, lakini tumesema msingi wa kuweza kushughulikia tatizo hili vizuri na kikamilifu ni kufanya marekebisho ya sheria. Kwa sababu kufanya kitu chochote kile nje ya sheria kwa ajili tu ya kutaka kujibu hoja za makundi au za mtu mmoja mmoja ni jambo ambalo halitaweza kutufanya tukafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nashauri Mheshimiwa Mbunge na wadau wengine wote na Taifa kwa ujumla tufanye subira. Tusubiri mabadiliko ya sheria ambayo yataweka misingi sasa ya kuweza kutatua changamoto hizi kwa namna ambayo itakuwa ni endelevu.

**SPIKA:** Sasa tunaelekea Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, swali linaulizwa na Mheshimiwa Boniphace Getere, Mbunge wa Bunda.

Na. 3

### **Wakulima wa Pamba Kupata Zao Mbadala**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE** aliuliza:-

Zao la pamba ndilo zao kuu katika Wilaya ya Bunda:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwapatia zao mbadala wakulima wa zao la pamba, baada ya zao hili kuelekea kutokomea kutokana na matatizo ya bei ndogo isiyokidhi mahitaji ya uzalishaji wake?

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza uzalishaji wa zao la pamba hasa ikizingatiwa kuwa Wilaya ya Bunda yenye majimbo matatu inategemea viwanda vya pamba katika mapato na ajira?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali bado inaona kuwa kuna tija katika zao la pamba kwa wakulima wa Bunda na maeneo mengine yanayolima pamba nchini kuliko mazao mengine kwa manufaa ya wakulima wenyewe na Taifa kwa ujumla. Hata hivyo, wakulima wanaweza kulima pamba sambamba na mazao mengine kama vile mazao ya bustani ili kujiongezea kipato. Aidha, kuyumba kwa uzalishaji wa pamba hapa nchini kunasababishwa na changamoto nyingi ikiwemo mabadiliko ya mara kwa mara ya bei katika soko la dunia, kukosekana kwa mbegu bora, upatikanaji na matumizi sahihi ya viuatilifu na mbolea.

Mheshimiwa Spika, hali hii imefanya wakulima wengi wa pamba nchini kuzalisha wastani wa kilo 300 kwa ekari tofauti na kilo 800 zinazopaswa kuzalishwa kwa ekari. Ili mkulima aweze kuona faida ya kilimo cha pamba anayouza kulingana na bei inayopangwa na wadau wakiwemo wakulima, mkulima anatakiwa azalishe zaidi ya kilo 800 kwa ekari ya pamba nyuzi yenye ubora unaotakiwa na soko.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali imeandaa mpango maalum wa kuhakikisha kuwa kufikia msimu wa 2018/2019 wakulima wa pamba kote nchini wanatumia mbegu bora za pamba aina ya *UKM08* zenye tija kubwa badala ya mbegu aina ya *UK91* ambayo imepoteza ubora wake. Mbegu hiyo ya *UKM08* inazalishwa katika maeneo ya Meatu, Nzega na Igunga ambayo hayana ugonjwa wa mnyauko. Aidha, Serikali inaendelea kusimamia upatikanaji wa viuatilifu bora na matumizi sahihi ili kuhakikisha wakulima wanatumia na kupata pamba iliyo bora na kukidhi mahitaji ya soko.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Serikali imeandaa mkakati wa kitaifa wa *Cotton To Clothing* 2016 – 2020 wenye lengo la kuendeleza mnyororo wa thamani wa zao la pamba ambao utaondoa utegemezi wa bei ya soko la kimataifa kwa kuwekeza katika viwanda vitakavyonunua pamba ya wakulima na hivyo kupunguza uuzaji wa pamba ghafi nje ya nchi. Hatua hii inakwenda sambamba na malengo ya Kitaifa ya kuwa nchi ya viwanda.

**SPIKA:** Maswali ya nyongeza, Mheshimiwa Boniface Mwita Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza maswali ya nyongeza mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tatizo la upatikanaji wa pembejeo kwa zao la pamba ni la muda mrefu sana karibu miaka 17 au 20. Ni lini sasa Serikali itakuwa na mikakati maalum ya kumaliza tatizo hili la pembejeo kwa wakulima wa pamba kwa sababu limekuwa sugu kwa muda mrefu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; ni muda mrefu sana Serikali tumekuwa tukipandisha bei ya pamba kwa kutegemea soko la dunia. Ni lini sasa Serikali itatengeneza mkakati wa kupata bei ya wakulima wa pamba kwa kutegemea soko la ndani?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuboresha upatikanaji wa pembejeo za pamba. Hatua mojawapo ambayo imeshafanyika ni kuanzishwa kwa Mfuko Maalum wa Wakfu wa Pamba (CDTF), ambao kazi yake kubwa ni kugawa na kuhakikisha pembejeo

zinapatikana kwa bei nafuu kwa wakulima wa pamba, kazi ambayo tayari imekuwa ikiendelea kwa miaka kadhaa sasa.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile Serikali inaendelea na mpango wa kuvifufua na kuboresha utendaji wa vyama vya ushirika ili viweze kusimamia upatikanaji wa pembejeo katika maeneo hayo. Jitihada hizi zinahusisha kwa mfano kufufua Chama cha Ushirika cha Nyanza ili kiweze kufanya kazi kuwasaidia wakulima wa pamba lakini vilevile vyama vingine kama *SHIRECU*, navyo vilevile kazi ya kuvifufua inaendelea.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na namna gani Serikali inaendelea kuboresha soko la ndani, napenda kumtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba, mkakati tulionao kwa sasa ni ule wa mwaka 2016-2020 wa kujaribu kuhakikisha tunaboresha mnyororo mzima wa thamani kutoka kwenye pamba hadi kufikia kwenye nguo. Katika mkakati huo, Serikali inahakikisha kwamba tunajenga viwanda na kuhamasisha ujenzi wa viwanda ndani ili nguvu kubwa isielekezwe tena katika kutafuta soko la nje bali kutumia soko la ndani ambalo tunaamini tunalo. Kwa sababu kwa idadi ya Watanzania iliyopo kama tutaweza kutengeneza nguo ambazo zitatumika ndani, tunaamini kwamba bei ya pamba itaendelea kuimarika.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Munde Tambwe, swali la nyongeza.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa, zao la pamba linafanana kabisa na matatizo ya zao kubwa la tumbaku la Mkoa wa Tabora; na kwa kuwa, Mkoa wetu wa Tabora unategemea sana zao la tumbaku. Zao la tumbaku limekuwa na tozo kuanzia 19 mpaka 38 zinazomuumiza mkulima wa tumbaku na kusababisha mkulima huyu faida yake yote kwenda kwenye matozo 38. Je, Serikali ina mpango mkakati gani wa

kuhakikisha inapunguza tozo hizi ili mkulima wa tumbaku apate faida kama ilivyopunguza tozo kwenye kilimo cha korosho? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:**

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, kati ya changamoto ambazo wakulima wa mazao hapa nchini wanapata ni tozo nyingi ambazo zinaendelea kuongeza changamoto kubwa katika uendeshaji wa kilimo. Namwomba Mheshimiwa Mbunge asubiri kusikia hotuba ya bajeti yetu kwa sababu mwaka huu wa fedha unaokuja, Wizara imeamua kuondoa karibu nusu ya tozo zote ambazo ziko kwenye mazao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sitaki kuwahi kuanza kueleza yaliyoko kwenye hotuba yetu ya bajeti, lakini nimweleze tu kwamba Serikali tayari ilishatambua changamoto hiyo; viongozi wetu wakuu, Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu kila wakati wamesisitiza kwamba tuondoe tozo hizo. Kwa sasa Wizara imeondoa tozo kwa 50% lakini kama ninavyosema tukija na maelezo yetu ya bajeti ataona ni tozo gani zimepungua.

Mheshimiwa Spika, vilevile Mheshimiwa Mbunge atakumbuka kwamba, hivi karibuni katika jitihada za kuondoa changamoto zilizopo kwenye zao la tumbaku (Tabora), Mheshimiwa Waziri Mkuu alienda kule na anajua yaliyotokea kule. Sasa changamoto ya chama kikubwa cha *WETCU* kuweza kuhudumia vizuri wakulima tayari inashughulikiwa pamoja na mambo mengine kwa kugawa iwe ni vyama viwili lakini vilevile ubadhirifu ambao umefanyika tayari wahusika wameshachukuliwa hatua.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kimsingi kuna mikakati mingi ambayo inaendelea ya kuhakikisha kwamba tunaboresha zao la tumbaku. Vilevile nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba Jumamosi hii tumeitisha



Mkutano wa Wadau wa Tumbaku na nachukua nafasi hii kumkaribisha tarehe 7 kwenye huo mkutano ili aangalie ni mikakati gani mbayo tumeweka. Nashukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Bado tuko Wizara hiyo hiyo Waheshimiwa Wabunge na muda hauko upande wetu, sasa nimruhusu Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya aulize swali lake kwa Wizara hii.

Na. 4

### **Mkakati wa Kuimarisha Sekta ya Kilimo**

**MHE. LEAH J. KOMANYA** aliuliza:-

Serikali imeweka kipaumbele kwenye sekta ya kilimo na kuainisha kwamba mazao ya kilimo yatakuwa moja ya malighafi kwenye viwanda nchini:-

(a) Je, Serikali imeweka mkazo gani kwenye vyanzo vya kilimo ambavyo ndivyo vitakuwa malighafi na kusababisha uzalishaji ukue?

(b) Je, Serikali ina mkakati gani juu ya uhakika wa wakulima wengi zaidi kuingia kwenye kilimo cha umwagiliaji?

(c) Je, Serikali imewekeza kwa kiasi gani kwenye zana za kilimo za kisasa kwa wakulima wadogo na hasa wanawake waishio vijijini?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mchango wa Serikali kwenye sekta ya kilimo ni pamoja na:-

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

(i) Kutoa ruzuku ya pembejeo za kilimo kwa wakulima ili kuongeza uzalishaji na tija.

(ii) Kutoa elimu ya kilimo bora kwa kutumia mashamba darasa 16,786 na mashamba darasa 44 ya vijana yaliyoanzishwa.

(iii) Kutumia Vituo vya Rasilimali vya Kata 587.

(iv) Kuanzishwa kwa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ili kuimarisha soko la mazao ya kilimo.

(v) Kukarabati maghala ya kuhifadhia mazao katika Halmashauri ambapo hadi sasa maghala 33 yamekamilika na maghala haya yatanufaisha wakulima wadogo 13,800 kwa kuhifadhi mazao yao.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuweka mikakati ya muda mfupi na muda mrefu ili wakulima wengi zaidi waingie kwenye kilimo cha umwagiliaji. Mikakati ya muda mfupi ni pamoja na:-

(i) Kukarabati na kuziboresha skimu za umwagiliaji 37 zenye ukubwa wa hekta 28,612.

(ii) Kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya umwagiliaji kwa njia ya matone.

(iii) Kuanzisha na kuimarisha vyama vya wamwagiliaji 442 katika skimu za wakulima wadogo.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali imetekeleza mikakati mbalimbali kwenye zana za kilimo kwa wakulima wadogo na hasa wanawake waishio vijijini ili kuwarahisishia kazi shambani. Kwa mfano, hadi sasa kuna matrekta makubwa 10,283 na matrekta madogo ya mkono 7,350. Wizara kupitia Mradi wa Sera na Maendeleo ya Rasilimali Watu (*Policy and Human Resource Development*) imesambaza mashine za kuvuna mpunga 64, kukata mpunga 16 na

mashine za kukoboa mpunga 14 katika skimu 14 za umwagiliaji. Mashine hizo zilizosambazwa zitasaidia kuongeza tija na kurahisisha kazi mashambani hususani kwa wanawake.

**SPIKA:** Swali la nyongeza, nimekuona Mheshimiwa Msukuma.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, bado sijauliza maswali yangu ya nyongeza.

**SPIKA:** Samahani Mheshimiwa, unajua watu wa Simiyu hawaonekani hapa. Mheshimiwa Komanya, tafadhali!  
(*Kicheko*)

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa, zana alizozitaja Mheshimiwa Naibu Waziri zinatumiwa zaidi na wanaume na zinarahisisha zaidi kazi kwa wanaume, hususan, kwenye kaya zenye uwezo. Je, Serikali ina mkakati gani wa kutoa zana ambazo zitamrahisishia mwanamke kulima mwenye kipato duni kama ninavyomwona mwanamke aishiye Mkoa wa Simiyu?  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili. Ilani ya Chama cha Mapinduzi imekusudia kutoa ajira zaidi. Kwa kupitia malighafi za mazao, si tu ajira zitatoka katika viwanda bali pia katika mazao ambayo yatauzwa na wakulima. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha inatoa mbegu ambazo zitaleta tija katika kilimo cha mtama na alizeti katika Mkoa wa Simiyu?  
(*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Majibu kwa kifupi, Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa William Tate Olenasha.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, jitihada mbalimbali ambazo Serikali inachukua kuboresha kilimo za kugawa na kuleta zana za kilimo zinawasaidia wakulima wote wakiwemo na

wanawake. Tunaamini kwamba tukiweza kuwa na zana za kilimo za kisasa, wanufaika wa kwanza watakuwa ni wanawake kwa sababu wao hasa ndio kwa kiasi kikubwa wanajihusisha na kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile Wizara kupitia Mfuko wa Pembejeo imeweka utaratibu wa kuweza kukopesha zana za kilimo kwa bei nafuu na wanawake kwa kupitia vyama vya ushirika lakini vikundi mbalimbali ni wanufaika wakubwa wa huduma hii. Vilevile Wizara kwa kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo inatoa mikopo kwa ajili ya pembejeo. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge aweze kuwasiliana na sisi ili kuwaunganisha akinamama wakulima wa Simiyu ili waweze kupata huduma hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na kugawa mbegu za mtama na alizeti, katika mwaka wa fedha unaokwisha na hasa baada ya changamoto ya mvua kutokuwa nzuri, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iligawa zaidi ya mbegu milioni 14 za mtama. Vilevile tumegawa mbegu za alizeti kwa wakulima mbalimbali nchini wakiwepo na wakulima wa Mkoa wa Simiyu.

**SPIKA:** Nilishakutaja Mheshimiwa Musukuma, swali fupi la nyongeza.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa kuwa matatizo yaliyopo Simiyu yanafanana sana na matatizo yaliyopo Mkoa wa Geita na Kagera, Serikali imetangaza wafugaji watoke kwenye Pori la Kimisi na Burigi na wakatii sheria. Sasa wale askari wanaoendesha ile operesheni wanazifuata ng'ombe vijijini kilometa saba mpaka kumi na kuzirudisha porini na baadaye kuwafilisi wananchi hawa. Je, ni nini kauli ya Waziri kuhusiana na uonevu unaoendelea kule Burigi na Kimisi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu kwa kifupi Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama alivyoeleza kwamba tayari

katika zoezi linaloendelea la kuondoa mifugo katika misitu na hifadhi kuna changamoto ambazo zimeripotiwa. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara imepokea changamoto hizo na inaendelea kujadiliana ndani ya Serikali kuangalia namna ya kuzitatua kwa muda mfupi.

**SPIKA:** Ahsante sana. Tuelekee Wizara ya Nishati na Madini, swali la Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mbunge wa Kwela.

Na. 5

### **Uchimbaji wa Gesi ya *Helium* – Rukwa**

**MHE. IGNAS A. MALOCHA** aliuliza:-

Serikali ilituthibitishia kuwa gesi aina ya *Helium* iligundulika katika Ziwa Rukwa na kwamba gesi hiyo ina thamani kubwa na ni adimu sana duniani:-

Je, ni lini sasa Serikali itaanza kuchimba gesi hiyo ili Watanzania waanze kunufaika na gesi hiyo kabla hajagunduliwa au kuchimbwa mahali pengine duniani?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kampuni ya *Helium One Limited* imefanya utafiti wa gesi ya *Helium* katika Bonde la Ziwa Rukwa. Taarifa za awali zinaonesha uwezekano wa kuwepo kwa gesi ya *Helium* kiasi cha futi za ujazo bilioni 54 katika maeneo ya Ziwa Rukwa. Matokeo haya yanatokana na uchunguzi wa sampuli tano za mavujia ya gesi ya *Helium* katika maeneo hayo, kiasi ambacho kinakadiriwa kuwa kikubwa zaidi ya mara sita ya mahitaji ya dunia kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *Helium One Limited* imefanya utafiti huo kupitia kampuni zake tanzu za *Gogota (TZ) Limited, Njozi (TZ) Limited* na *Stahamili (TZ) Limited* zinazomiliki leseni za utafutaji wa gesi ya *Helium* katika Ziwa Rukwa. Kampuni hizi zilipewa leseni za utafutaji wa *Helium* katika maeneo mbalimbali kuanzia mwaka 2015. Shughuli za utafutaji wa kina wa gesi ya *Helium* unaendelea kwa kukusanya taarifa zaidi za kijiolojia, kijiokemia, kijiofizikia na *2D* ili zitumike kwa ajili ya uchorongaji wa visima vya utafiti wa gesi asilia kilichopo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, uchimbaji wa gesi ya *Helium* utanza mara baada ya kazi ya utafiti wa kina, upembuzi yakinifu na tathimini ya athari za mazingira kukamilika. Baada ya utaratibu kukamilika, uchorongaji katika maeneo ya Ziwa Rukwa unatarajiwa kuanza mwaka 2018.

**SPIKA:** Mheshimiwa Malocha, swali la nyongeza.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri na ufafanuzi wa swali langu la msingi umeeleweka lakini ninayo maswali mawili ya nyongeza. La kwanza, ni lini Serikali itapeleka umeme wa *REA III* katika Jimbo la Kwela? Nauliza hivyo kwa vile Ukanda wa Ziwa Rukwa haujaguswa kabisa karibu Kata 13 na Kata saba za Ukanda wa Juu na zenyewe hazijaguswa kabisa, jumla Kata 20 hazijaguswa hata kijiji kimoja.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ni lini Serikali itamalizia kupeleka umeme katika *REA III* katika vijiji 68 ambavyo havijapelekewa umeme katika Kata za Mpwapwa, Jangwani, Mpuhi, Likizi, Kalambanzite, Lusaka, Lahela na Sandurula? (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Malocha, swali limeeleweka. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Dkt. Kalemani

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Malocha kwa jinsi anavyofuatilia masuala ya umeme kwa wananchi wa Jimbo lake. Mheshimiwa hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ni lini Serikali itapeleka umeme katika Kata zake 20 ambazo zimebaki, kwanza kabisa tunakubaliana na Mheshimiwa Malocha kati ya Kata 27 zilizopata umeme ni Kata mbili ziko katika Jimbo lake. Kwa hiyo, Kata 25 zilizobaki kama ambavyo ameeleza ikijumlishwa pia Kata zake za Kipeta, Kilangawani, Kigamadutu pamoja na Malegesya na shule za sekondari alizozitaja zitapatiwa umeme kupitia mradi wa *REA* ambao umeanza kutekelezwa nchi nzima mwezi huu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimpe uhakika Mheshimiwa Malocha kwamba Kata zake zote 27 na zile mbili ambazo zimepata bado Vitongoji vyake navyo vitapelekewa umeme kuanzia mwezi huu hadi miaka minne ijayo. Kwa hiyo, tuna uhakika Kata zako 27 Mheshimiwa Malocha zitakuwa zimepata umeme wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na vijiji 68, ni kweli kabisa vipo vijiji 68 katika Jimbo la Mheshimiwa lakini na vitongoji 237. Tunapopeleka umeme katika vijiji 68 katika Jimbo la Kwela tunapeleka pia katika vijiji 237 ambapo vitongoji vyake vyote havijapata umeme.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Malocha vitongoji vyake vyote ambavyo havijapata umeme vile vya Mpwapwa, Muze, Halula na Mwandui vyote vitapata umeme. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, swali la Mheshimiwa Mwalimu Kasuku Samson Bilago.

Na. 6

**Wananchi wa Kakonko Kulipwa Fidia ya  
Kuvunjiwa Nyumba Zao**

**MHE. KASUKU S. BILAGO** aliuliza:-

Kwa muda wa miaka tisa sasa baadhi ya wananchi wa Wilaya ya Kakonko nyumba zao zimewekwa 'X' kwa lengo la kuvunjwa ili kupisha ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami:-

(a) Je, ni wananchi wangapi kati ya hao wenye alama ya 'X' kwenye nyumba zao wanakidhi vigezo vya kulipwa na sababu ni zipi kwa wasiolipwa?

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha kitatumika kulipa fidia nyumba hizo?

(c) Je, fidia hiyo itazingatia gharama ya nyumba kwa sasa au gharama ya zamani ya nyumba zilizowekwa 'X' na ni lini watalipwa?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA  
MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kasuku Samson Bilago, Mbunge wa Buyungu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, eneo la Kakonko ni mojawapo ya maeneo yanayopitiwa na barabara kuu inayopitia Tunduma – Sumbawanga – Mpanda – Kanyani – Kasulu – Kibondo – Kakonko hadi Nyakanazi. Alama za 'X' ziliwekwa ili kubainisha wananchi waliojenga ndani ya hifadhi ya barabara ambayo ina upana wa mita 30 kutoka katikati ya barabara kila upande.



Mheshimiwa Spika, hakuna mwananchi anayekidhi vigezo vya kulipwa nyumba iliyowekwa 'X' kwani nyumba hizo ziko ndani ya hifadhi ya barabara yaani ndani ya mita 22.5 kutoka katikati ya barabara kwa mujibu wa Sheria ya Barabara ya mwaka 1967 na nyongeza ya hifadhi ya barabara ya mita 15 yaani mita 7.5 kila upande kwa mujibu wa Sheria ya Barabara ya mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hakuna nyumba iliyofuatwa na barabara, hakuna fedha ya fidia kwa ajili ya nyumba hizo. Aidha, kuna mashamba 99 ambayo yamo ndani ya hifadhi ya barabara iliyoongezwa ya mita 7.5 ambayo yatalipwa fidia kulingana na sheria zilizopo.

**SPIKA:** Ahsante sana Injiniya Ngonyani, Mwalimu Bilago swali la nyongeza.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nisikitike kwa majibu yaliyotolewa na Wizara juu ya swali hili, haya siyo majibu sahihi kwa swali hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Mji wa Kakonko nyumba zinazozungumziwa zilikuwepo kabla ya mwaka 1967 kwa sheria iliyotungwa. Haiwezekani *survey* inayofanyika ikafanyika na kukuta hakuna nyumba hata moja inayokidhi vigezo vya kulipwa. Kwa maelezo hayo, Serikali ya Chama cha Mapinduzi imepanga kuwatia umaskini wananchi katika Mji wa Kakonko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *survey* ile inaonesha tangu miaka tisa iliyopita hakuna aliyekuja kuzungumzia kwamba nyumba zile hazitalipwa. Wananchi wamekuwa wakipigwa picha wanapewa matumaini ya kulipwa leo taarifa inakuja hawawezi kulipwa. Sasa nauliza, je, ana uhakika kwamba hakuna nyumba iliyokuwepo kwa sheria iliyokuwepo kabla ya mwaka 1967?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa majibu hayajakidhi vigezo vya nyumba zilizopo katika eneo hilo

ambazo zitabomolewa na zote hazina vigezo, Serikali iko tayari kwenda kufanya *survey* upya katika Mji wa Kakonko na kujiridhisha kwamba zipo nyumba ambazo zinakidhi vigezo na hivyo wananchi wake waweze kulipwa? (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mwalimu. Majibu ya maswali hayo kwa kifupi sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Injiniya Ngonyani.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, hizi sheria tunatunga wenyewe humu ndani ya Bunge. Sheria ya siku za nyuma toka mwaka 1932 mpaka ilipokuja kurekebishwa mwaka 1967 na sasa tunayo ya mwaka 2007 zote zilitungwa ndani ya Bunge. Naomba sana ndugu zangu tuheshimu kile ambacho tulikubaliana wote ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, naomba kurudia jibu langu la msingi kwamba katika barabara hiyo *survey* imefanyika na hakuna nyumba ambayo ipo nje ya mita 22.5 kwa sheria ya 1967 na nje ya mita 7.5 ya nyongeza kwa sheria ya mwaka 2007. Kwa hiyo, kurudia *survey* wakati mwingine tunapoteza fedha lakini kama kutakuwa na tatizo mahsusi, naomba Mheshimiwa Bilago awasiliane na meneja *TANROAD* Mkoa halafu tutaanzia hapo. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Nimemwona Mheshimiwa Nape Nnauye. (*Makofi*)

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa utaratibu wa kuweka 'X' kwenye nyumba au shughuli ambazo zinafanywa na wananchi kwenye maeneo ambayo Serikali inataka kuweka miundombinu ni utaratibu ambao sasa umezagaa nchi nzima. Kwa kweli unaathiri sana maendeleo ya wananchi

wetu kwa kuwa utaratibu huu unazuia wananchi kuendeleza maeneo yao na inachukua muda mrefu kwa Serikali kuanza kutekeleza mipango yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa, je, Serikali haioni kwamba umefika wakati wa kuubadilisha utaratibu huu wawe wanapanga mipango yao wakikamilisha ndiyo waende kuzungumza na wananchi kwenye maeneo husika? Mfano mzuri ni kwenye maeneo ya Jimbo langu la Mtama ambako inasemekana utapita mradi wa reli, zimewekwa 'X' kwa muda mrefu. Kama Serikali itakubaliana na utaratibu huu wa kubadilisha sasa utaratibu watoe tamko hapa niwaambie wananchi wangu wapige chokaa waendeleze maeneo yao. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri, Mheshimiwa Injinia Ngonyani.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, kama mtagundua sasa hivi kila barabara inayojengwa tunaweka mawe mita 30 kila upande ili tusisubiri wakati wa kupanua barabara. Watu wajue toka mwanzo kwamba barabara hifadhi yake ni mita 30 kila upande. Tatizo lililojitokeza siku za nyuma hizo alama zilikuwa haziwekwi kwa hiyo watu walikuwa wanavamia hifadhi ya barabara wengine kwa kujua na wengine kwa kutokujua.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa sasa ni kweli baada ya kupitishwa hii sheria mwaka 2007 tumeamua kuweka alama mita 30 kila upande na yeyote aliye katika eneo hilo tunamwekea 'X' ajue kwamba yupo ndani ya hifadhi ya barabara na hivyo anatakiwa aondoke. Sio suala la kufidia, wale wenye haki ya kufidiwa, wanakuja kufidia wakati kutakuwa na mradi maalum utakaopita mahali hapo na hatimaye fedha zinapopatikana. Hiyo ndiyo dhana ya kuweka alama hizi za mita 30 na tumefanya hivyo nchi nzima.

**SPIKA:** Tunaendelea Waheshimiwa na swali la Mheshimiwa Joyce Biti Sokombi.

Na. 7

## Ujenzi wa Barabara ya Tarime - Serengeti

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI** aliuliza:-

Barabara ya kutoka Tarime kwenda Serengeti ni barabara muhimu sana kwa wakazi wa Wilaya hizo na kwa maisha yao ya kila siku:-

Je, ni lini barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joyce Bitta Sokombi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Tarime – Serengeti ni barabara inayojulikana kwa jina la Tarime – Nyamwaga - Mugumu yenye urefu wa kilometa 87.14 ambayo inaunganisha Wilaya za Tarime na Serengeti.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Tarime – Nyamwaga – Mugumu (Serengeti) ni barabara inayohudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) Mkoa wa Mara. Kwa kuzingatia umuhimu wa barabara hii, Wizara kupitia *TANROADS* imekuwa ikijenga kwa kiwango cha lami kwa awamu kutokea Tarime Mjini hadi Kibumayi ambapo kilometa saba zimekamilika. Vilevile, katika mteremko wa Nyamwaga kuelekea mgodi wa Nyamongo kilometa 0.6 zimekamilika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2016/2017, ujenzi wa kilometa 2.2 unaendelea katika maeneo ya Kibumayi na mteremko wa Nyamwaga. Aidha, ujenzi wa daraja la Mto Mara lenye urefu wa mita 94 na ujenzi kwa

kiwango cha lami wa barabara unganishi ya kilometa 1.8 unakaribia kuanza kwa sababu mkandarasi amekwishapatikana na yupo katika maandalizi ya kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na ujenzi huo unaoendelea, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa barabara yote yenye urefu wa kilometa 87.14 unaendelea na unatarajiwa kukamilika Septemba, 2018. Hivyo, ujenzi wa barabara hii yote kwa kiwango cha lami unatarajiwa kuanza pindi kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zitakapokamilika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joyce Sokombi, swali la nyongeza.

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Majibu ya Waziri hayajaniridhisha. Barabara hii ina umuhimu mkubwa kwani hutumiwa na watalii wengi wanaotoka Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Jomo Kenyatta kuja *Serengeti National Park*. Je, hamuoni kwamba tunapoteza watalii wengi kutokana na ubovu wa barabara hii?

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa niliyoipata ni kwamba barabara hii ilikuwa iishe 2017, lakini nashangaa kwa majibu ya Waziri kwamba barabara hii inaisha 2018. Sasa nataka nijue barabara hii inaisha 2017 au 2018? Je, upembuzi yakinifu unaisha 2017 au 2018? Je, kwenye bajeti 2017 barabara hii imetengewa bajeti?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Injiniya Ngonyani.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii unaisha mwaka 2018 kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi. Nimhakikishie Mheshimiwa Sokombi kwamba hicho tunachokisema ndicho tutakachokitekeleza na umuhimu wa barabara hii umetokana na hao watalii wengi ambao wameanza kuonekana. Tunataka barabara hii pamoja na hiyo nyingine,

kama unavyofahamu tunajenga barabara nyingine ya kutoka Sanzatu, zote hizi tutazijenga kwa ajili ya kufungua utalii. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge hawa watalii mara baada ya kukamilisha kujenga barabara hizi wataongezeka.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, swali fupi sana la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kweli niendeleo kusikitika kwamba Serikali inashindwa kuona barabara ambazo zinaweza zikaongeza chachu ya ukuaji wa uchumi kwenye nchi yetu kupitia utalii.

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua ni lini Barabara ya Tarime – Nata kwa maana ya kwenda Mugumu itakamilika kwa kiwango cha lami? Mheshimiwa Naibu Waziri anatueleza kwamba upembuzi yakinifu unakamilika 2018, watalii wengi wanaotoka Kenya wanapita Tarime wanaenda Serengeti, tukiboresha ile barabara kwa kiwango cha lami tutakwenda kukuza uchumi wetu kwa sababu watalii wengi watapita kwa sababu barabara inapitika. Ni lini sasa Serikali itaji-*commit*, isiseme leo itamaliza upembuzi yakinifu 2018, ione kuna uhitaji wa haraka sana wa kujenga barabara ya Tarime – Mugumu na iweze kumalizika ndani ya mwaka mmoja kama ikiwezekana tuweze kukuza uchumi wa nchi yetu? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo kwa kifupi sana, Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, katika ujenzi wa barabara tuna hatua tatu muhimu na hatua hizi ni lazima zikamilike. Hatua ya kwanza ni upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Baada ya Serikali kuiona barabara hii kwamba ina umuhimu na inaongeza mapato yetu katika utalii imeamua kuanza hiyo kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Kazi hiyo itakamilika mwaka 2018.

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kazi hiyo kukamilika, hatua ya pili itakayofuata ni kutafuta fedha za ujenzi wa barabara hiyo. Huwezi ukajenga barabara bila fedha. Kwa hiyo, Serikali itatafuta fedha ili tuanze kujenga barabara hiyo. Tukishapata fedha tutatangaza tumpate mkandarasi wa kuanza kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, swali linaulizwa na Mheshimiwa Bhagwanji Maganlal.

Na. 8

**Haki ya Baba Kumuona Mtoto Pindi  
Wazazi Watenganapo**

**MHE. BHAGWANJI MAGANLAL MEISURIA** aliuliza:-

Inapotokea wazazi wametengana na mama akaondoka na mtoto na kwenda kuishi naye, lakini tangu wazazi hao watengane mama hatoi nafasi kwa baba kwenda kumtembelea mtoto:-

Je, baba ataipata wapi haki hiyo ya kumwona mtoto?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,  
JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Bhagwanji Maganlal Meisuria, Mbunge wa Jimbo la Chwaka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mtoto Namba 21 ya mwaka 2009 imezingatia suala zima la utoaji wa malezi, matunzo na ulinzi wa mtoto kwa kutoa majukumu kwa wazazi, walezi pamoja na Serikali. Kifungu cha 7(1) cha sheria hii kimempa mtoto haki ya kuishi na wazazi wake au kuishi na

mlezi. Aidha, kifungu cha 26(1) kimeeleza haki za mtoto endapo wazazi watakuwa wametengana. Haki hizo ni pamoja na kuendelea kupewa matunzo pamoja na elimu kama ilivyokuwa kabla ya wazazi kutengana, kuishi na mzazi mmojawapo baada ya mahakama kujiridhisha kuwa mzazi huyo anao uwezo wa kumlea mtoto. Pia mtoto kuwa na haki ya kumtembelea na kukaa na mzazi wake mwingine pale atakapotaka kufanya hivyo isipokuwa kama itabainika kuwa kumtembelea mzazi mwingine kutaathiri masomo na ustawi wa mtoto.

Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa zipo taratibu za kufuata endapo mzazi mmoja (baba au mama) atakosa haki ya kumwona mtoto wake ambaye anaishi na mzazi mwingine. Kwa mujibu wa taratibu, mlalamikaji atatakiwa kuripoti ofisi za Ustawi wa Jamii za Halmashauri pale ambapo mzazi mwenza anaishi na mtoto ili waweze kukutanishwa na kufanyiwa unasahi ili hatimaye waweze kufikia makubaliano ya pamoja ya kumlea mtoto.

Mheshimiwa Spika, aidha, pale inaposhindikana, mashauri haya huelekezwa kwenye Baraza la Usuluhishi lililoko chini ya Kamishna wa Ustawi wa Jamii na pindi wasipofikia makubaliano kwenye Baraza la Usuluhishi, shauri hupelekwa Mahakamani kwa hatua zaidi za kisheria.

**SPIKA:** Mheshimiwa Meisuria, swali la nyongeza.

**MHE. BHAGWANJI MAGANLAL MEISURIA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru Mheshimiwa Naibu Waziri amenijibu vizuri lakini nina maswali ya nyongeza. Ni kweli kabisa aliyosema, nakubali wazazi wote wapate haki kamili ya kumlea mtoto. Ikiwa mtoto yupo kwa mama aruhusiwe kwenda na kwa baba. Hata hivyo, katika Tanzania yetu wananchi wengi hawampi baba haki ya kumlea mtoto au hata kumwona, je, Serikali inasemaje kuhusiana na suala hili? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili. Huyu mtoto kuanzia miaka mitatu hadi saba yupo kwa mama, ikiwa



mtoto huyo amefikisha miaka saba, je, baba anayo haki ya moja kwa moja kumlea, kumsomesha na kumuangalia kiafya? Kwa sababu watoto wengi wa Tanzania hawapati nafasi ya kulelewa na baba. Kwa hiyo, baba apate nafasi ya kulea, baada ya miaka saba apewe mtoto. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana kwa swali hilo. Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, baba apewe mtoto unasemaje? (Kicheko)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, kupiga mimba haitoshi kukufanya uwe baba...

**WABUNGE FULANI:** Ee.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Yaani kumtia mwanamke mimba haitoshi kukufanya uitwe baba. Ili kuwa baba kamili, pindi unapompa mimba mwanamke unapaswa kwanza kuitunza mimba yenyewe, lakini baada ya hapo kumtunza mtoto baada ya kuzaliwa, muwe mnaishi pamoja ama hamuishi pamoja na huyo mwanamke. Hilo ni jukumu la kwanza unapokuwa mwanaume na imetokea umempa mimba mwanamke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama kuna mgogoro wowote ule unaoweza kutokea katika mchakato huu kuna taratibu za kufuatwa. Moja ya taratibu ni za kimila ambapo yanaweza yakatokea mashauriano ya kimila kwenye jamii kati ya upande wa baba na upande wa mama na wakaelewana kimila na kuna gharama za kutoa. Kwa mfano, kwa Wasukuma kuna ngwegwe na nafahamu kwenye makabila mengine pia kuna taratibu za kufuata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ikishindikana kimila ndiyo unafuata huo mchakato wa kisheria niliousema ambapo utapaswa kwanza kumpa haki mama kumlea mtoto mpaka miaka saba ifike na katika kipindi hiki cha miaka saba

unapaswa kuwa umemtunza yule mama. Pale mwanzoni kama hukumuoa huyo mwanamke unapaswa ukajitambulisha rasmi kwamba wewe unahusika na ile mimba, siyo umeikataa mimba halafu mtoto akizaliwa anafanana na wewe unasema mtoto ni wa kwako, hapana! (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwanza kwa mujibu wa sheria unapaswa ama ufuatae taratibu za kimila ujitambulisha kwamba wewe ndiye uliyetia mimba, uilee mimba na mwisho wa siku umlee mtoto au kwa taratibu za kisheria ujitambulisha mahakamani kwamba wewe ndiye umetia mimba na utailea. Sasa ikifika ile miaka saba una haki ya kudai mtoto. Nadhani Mheshimiwa Meisuria amenielewa. (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Ummy majibu ya nyongeza, pia tuhakikishie mtoto akifika miaka saba baba anaruhusiwa kumswaga kwenda naye?

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, nataka kuongeza hiyo sehemu ya pili.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto Na.21 ya mwaka 2009, *presumption* ni kwamba mtoto anatakiwa akae na mama *in the best interest of the child* lakini akifika miaka saba sheria inasema *in the opinion of the court* anaweza akakaa na mzazi yeyote pale mahakama itakapojiridhisha kwamba mtoto huyu atapata matunzo na malezi mazuri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Bhagwanji kwamba kama mtoto amefikisha miaka saba siyo lazima akae na mama, mahakama itapima na kuona *in the best interest of the child* mtoto huyu atapata malezi mazuri wapi, kwa baba au kwa mama. (Makofi)

**SPIKA:** Swali hili muhimu sana, tupate maswali mawili ya nyongeza hapa. Niliwaona Mheshimiwa Maryam Msabaha na Mheshimiwa Jaku. Mheshimiwa Maryam Msabaha.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nami naomba nimuulize Naibu Waziri swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa ongezeko la watoto wa mitaani linachangiwa na akinababa kukataa mimba na kukataa familia zao. Je, Serikali inaweza kusema mpaka sasa hivi ni akinababa wangapi wameshatiwa hatiani na kufunguliwa mashtaka ili kutunza familia zao? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri hawezi kuwa na takwimu za wangapi, lakini pia na akinamama wangapi wamechukuliwa hatua, mbona hilo hukuliweka? Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, kwanza hatuna takwimu sahihi za watu waliochukuliwa hatua kwa kukataa mimba. Hata hivyo, nimhakikishie tu kwamba tuko makini katika kufuatilia kesi za namna hiyo ili kuweza kuchukua hatua pindi inapojitokeza.

**SPIKA:** Ahsante sana. Nilikutaja Mheshimiwa Jaku.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nami kwanza kabla ya yote niungane na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kumtakia afya njema Mheshimiwa Rais Mstaafu Dkt. Jakaya Kikwete pamoja na familia yake kwa jinsi alivyotuongoza kipindi chake. Pamoja na hayo, naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

**WABUNGE FULANI:** Moja.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Basi nitauliza swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri na Waziri wake kwa kuwa makini wakati wa kujibu suala hili lakini kuna kadhia kama hii imetokea kwa baba kufariki na watoto kubaki na huyu mtu akaenda kulalamika Ustawi wa Jamii nao wakapendekeza kwamba watoto hawa ikifika muda waende kwa babu yao na ukitazama chimbuko la hawa watoto ni babu. Leo kwa nini babu ananyimwa haki yake ya kuwasomesha watoto wale? La kushangaza, baadaye bibi huyo akakimbilia mahakamani nayo ikaamua kuwa shule zikifungwa wakatembelee tu watoto asiweze kuwachukua. Haki ya mtoto iko wapi hapo katika vifungu ulivyotaja 21 na 7?

**SPIKA:** Majibu mafupi ya swali hilo, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, Naibu Waziri wa Afya.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mtoto iko wazi katika kifungu cha 37 ambacho kinahusu *custody of the child*. Katika kifungu hicho utaratibu unawekwa kwamba pale mtoto anapokuwa amefika umri wa miaka saba utaratibu unabadilika badala ya kubaki tu kwamba atakuwa chini ya usimamizi wa mama yake sasa mahakama inaweza ikaamua mtoto ama aende kwa baba au kwa mama kwa kuzingatia mahali ambapo huyo mtoto atapata malezi bora.

Mheshimiwa Spika, lakini kama imetokea sasa mzazi ambaye ni baba amefariki, maana yake mzazi anayebaki *automatically* ni yule mmoja kwa sababu mtoto ni wa wazazi wawili. Kwa hiyo, kama mama yupo maana yake *naturally* tu mama anapata haki ya kumlea yule mtoto siyo tena kwa babu mzaa baba, hapana! Kama mama yupo lakini baba amefariki haki inabaki kwa mama.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama inatokea kwamba mama anaonekana hana uwezo wa kumlea yule mtoto ama mtoto hapati haki ama mtoto anafanyiwa vitendo vya ukatili kwa namna yoyote ile na wazazi na jamii ipo, basi hao wazazi kama babu wanaweza wakaenda

mahakamani kwenda kushtaki na shauri hili likajadiliwa pale na hatimaye mahakama itaamua kutafsiri kifungu hicho *in the best interest of the child*.

**SPIKA:** Ahsante. Swali la mwisho la leo, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela.

Na. 9

### **Ndoa za Utotoni**

**MHE. ANNE K. MALECELA** aliuliza:-

Ndoa za utotoni kwa sasa zimekithiri sana na ndoa hizi zina athari kubwa ndani ya jamii:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutokomeza ndoa hizi za utotoni?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua athari kubwa zanzosababishwa na ndoa za utotoni katika jamii yetu ya Tanzania. Ndoa za utotoni zinawanyima watoto wa kike fursa ya kupata elimu na hivyo kusababisha umaskini miongoni mwao punde wanapokuwa watu wazima kwa kuwa wanakosa mbinu mbadala za kujikwamua kiuchumi kutokana na kukosa elimu. Aidha, mimba za utotoni ni hatari kwa afya ya mama na mtoto kwa kuwa maumbile ya kibaiolojia ya mtoto hayawezi kuhimili mchakato wa uzazi na mara nyingi mimba hizi zimesababisha vifo.

Mheshimiwa Spika, kulingana na takwimu za afya na idadi ya watu nchini za mwaka 2016, ndoa za utotoni

zimeshamiri katika Mikoa ya Shinyanga kwa kiwango cha asilimia 59, Tabora kwa kiwango cha asilimia 58, Mara asilimia 55 na Dodoma asilimia 51.

Mheshimiwa Spika, kwa kukabiliana na changamoto hii, Serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwemo kutoa elimu ya malezi chanya kwa wazazi na walezi ili waweze kutambua umuhimu wa kumwendeleza mtoto wa kike. Elimu hii imetolewa katika Halmashauri za Wilaya, Manispaa na Miji 72 nchini. Msukumo umeongezwa zaidi katika kuelimisha familia, wazee wa mila na jamii kuachana na mila na tamaduni zilizopitwa na wakati za kuoza watoto wa kike. Mwaka 2015, Serikali ilizindua rasmi kampeni ya Kitaifa ya kutokomeza ndoa za utotoni ambayo iliwataka wadau wote zikiwemo familia kushirikiana kutokomeza kabisa ndoa za utotoni hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa muundo wa kiseria na kisheria, Serikali imezifanyia maboresho sera na sheria ili kumlinda mtoto wa kike dhidi ya ndoa na mimba za utotoni mfano Sera ya Elimu ya mwaka 2014 inaelekeza kutolewa kwa elimu bure na ya msingi kuanzia elimu ya awali mpaka kidato cha nne pamoja na marekebisho ya Sheria ya Elimu, Sura ya 353 yaliyopitishwa na Bunge la 11 ambayo inatoa adhabu ya kifungo kisichopungua miaka 30 kwa mtu yeyote atakayempa mimba mwanafunzi wa shule ya msingi au sekondari.

Mheshimiwa Spika, tarehe 13 Desemba, 2016, Serikali ilizindua mpangokazi wa Taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto uliojumuisha sekta zote zinazohusu wanawake na watoto kwa lengo la kutokomeza aina zote za ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Mpangokazi huu ambao utanza kutekelezwa mwezi Julai, 2017, umelenga zaidi kuzuia na kupunguza vitendo vyote vya ukatili dhidi ya watoto kwa asilimia 50 na umeweka lengo la kupunguza mimba za utotoni kutoka asilimia 47 hadi asilimia 10 ifikapo mwaka 2022.

**SPIKA:** Ahsante kwa majibu yako, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela swali la nyongeza.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na majibu ya Serikali, lakini naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, kwa mfano tu Wilaya ya Same mwaka 2016, wasichana wadogo waliopata mimba na kufukuzwa shule ni 64 ambao hawa ni wa *O-Level* ikiwa ina maana mimba hizi ni za utotoni. Mwaka huu 2017 mwezi wa Kwanza, wa Pili na wa Tatu, miezi mitatu tu wamefukuzwa wanafunzi wa shule kwa mimba za utotoni 42 na kati ya hao akiwepo mtoto wa darasa la sita ikiwa ina maana ni kati ya miaka 12 mpaka 14.

Mheshimiwa Spika, hivi Serikali haioni kwamba kuna umuhimu mkubwa sana wa kuwa na mitaala ambayo itawafundisha watoto hawa kuanzia shule ya msingi mpaka sekondari, ambayo itawafanya waelewe athari za kupata mimba utotoni ambazo ni muhimu sana? Mitaala hii itaweza kuwasaidia watoto hawa kujitambua na kufahamu umuhimu wa kutokukubali kupata mimba utotoni.

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa Serikali inafanya jitihada kubwa sana kupambana na madawa ya kulevya sasa hivi na naiunga mkono, *nai-support* na tunashukuru sana. Jitihada hii ni kwa sababu Serikali imeona athari hasa inayowapata vijana wa kiume na wa kike kwa kutumia madawa ya kulevya, lakini watoto wa kike wanapata athari mara mbili, kwanza athari ya madawa ya kulevya na mimba za utotoni.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuleta mkakati mkubwa kama ule wa madawa ya kulevya ili tupunguze athari za mimba za utotoni? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali linalohusiana na masuala ya mitaala kama ifuatavyo:-

Kimsingi katika elimu ya Msingi na elimu ya Sekondari wanafunzi wanapewa maarifa kuhusiana na masuala ya Kibaiolojia na sayansi yanayohusisha hata masuala ya maumbile ya miili yao, kwa hiyo kimsingi suala hilo linafanyika labda tunaloweza kuahidi hapa ni kutoa msisitizo wa kuona kwamba wanafunzi hao wanapewa dozi zaidi hasa kwa kuwachukua hawa watoto wa kike na kuwapa elimu ya ziada kwa ajili ya kuwanusuru katika mazingira hayo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya yale maswali mengine ya Mheshimiwa Mama Kilango, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya hasa kwa Wasukuma na Wanyamwezi kama walivyotamka wao wenyewe ambao ndiyo wanaongoza kutia mimba wanafunzi. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, na Wagogo wamo. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri endelea unaongea na mimi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, kwanza tunao mpango wa kudhibiti ukatili dhidi ya wanawake na watoto ambao ni jumuishi kwa sekta takribani tisa za Serikali yetu na mpango huu umezinduliwa mwaka jana mwezi Desemba na Mawaziri tisa wa Serikali hii ya Awamu ya Tano na Mawaziri wameonesha *comittment* kubwa sana ya kuweka utaratibu wa kumlinda mtoto wa kike dhidi ya ndoa za utotoni lakini pia mimba za utotoni na vitendo vyote vinavyohusu ukatili dhidi ya wanawake na watoto wa kike.

Mheshimiwa Spika, tunachokihitaji kwa sasa ni kupewa fedha kwa ajili ya kutekeleza mpango huo na



kwenye mpango huu tunalenga kupunguza vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto kwa kiwango cha asilimia isiyopungua 50 kufikia mwaka 2022. Kwa hivyo, mpango huu kama tutapangiwa fedha, tunapanga kuanza kuutekeleza mwezi Julai mwaka 2017. Kwa hivyo, mpango tunao pia tuna mikakati mbalimbali inayoendelea kama ya elimu ya malezi *chanya* (*Positive Parenting Education*) kwa watoto ambao umefanyika kwenye Wilaya 72 za Nchi yetu na tunawalenga zaidi viongozi wa kimila, wazazi pamoja na watu mashuhuri wenye kufanya maamuzi kwenye jamii.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda hauko upande wetu kabisa kabisa, nashukuru sana tumepata nafasi ya leo kupata maswali ya Wabunge 20, lakini nitawaomba tunavyozidi kwenda kwa sababu muda wetu ni saa moja mtaona jinsi tulivyopitiliza kweli kwa kipindi hiki, hivyo Waheshimiwa Mawaziri majibu yazidi kuwa mafupi zaidi na Waheshimiwa Wabunge wote maswali yaendeleo kuwa mafupi zaidi ili muda wetu utoshe.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii ni pamoja na mgeni aliyepo kwenye jukwaa la Spika, Mama Tunu Pinda mke wa Waziri Mkuu Mstaafu Mheshimiwa Mizengo Pinda, Mama Tunu amekuja kushuhudia kuapishwa kwa Mheshimiwa Salma Kikwete, karibu sana Mama yetu na tupelekee salamu kwa Mzee. (*Makofi*)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge kama mnavyoona *gallery* zimejaa tunawakaribisha wageni wetu wote kutoka popote pale katika nchi yetu karibuni sana Bungeni. Mheshimiwa Hamidu H. Bobali, Katibu wa tawi la *club* gani sijui hii!

**WABUNGE FULANI:** Yanga.

**SPIKA:** Eehhh, anasema wale wenzake wale mkutane katika ukumbi wa Msekwa B, Simba au nini hii?

**WABUNGE FULANI:** Yanga.

**SPIKA:** Aaahh ni Yanga. Mheshimiwa Hamidu H. Bobali, Katibu wa Wanayanga wa tawi anaomba mkutane Msekwa B. (*Makofi/Kicheko*).

Mheshimiwa Jasson S. Rweikiza, Katibu wa Wabunge wa CCM anaomba niwatangazieni Wabunge wa CCM wote kwamba kutakuwa na kikao cha *caucus* mara tu baada ya Bunge kuahirishwa asubuhi hii katika ukumbi wa *NEC* pale *White House*, Wabunge wote wa CCM mkutane *White House* mara tu baada ya kuahirishwa shughuli hizi asubuhi hii ya leo. Katibu.

**NDG. RAMADHAN ABDALLAH ISSA-KATIBU MEZANI:**

### **HOJA YA KUTENGUA KANUNI**

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WALEMAVU:** Mheshimiwa Spika, naomba nitoe hoja ya kutengua Kanuni za Bunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mkutano wa Saba wa Bunge umeanza leo tarehe 4 Aprili, 2017 na umepangwa kumalizika tarehe 30 Juni, 2017. Shughuli zilizopangwa kufanyika katika mkutano huu ni pamoja na uchanguzi wa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa shughuli zilizopangwa leo haziwezi kukamilika iwapo Bunge litarejea saa 11 jioni, kwa upande mwingine shughuli za Mkutano huu wa Saba hazitafanyika kwa ukamilifu iwapo vikao vya Bunge vitafanyika katika siku za kazi peke yake yaani Jumatatu mpaka Ijumaa, hivyo basi naomba Bunge lako liridhie Kanuni ya 28(2) itenguliwe ili leo tarehe 4 Aprili, 2017 Bunge likisitishwa lirejee tena saa 10 jioni badala ya saa 11 jioni ili kuruhusu Bunge kufanya uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki na Kanuni ya 28(15) itenguliwe ili kuruhusu baadhi ya siku za Jumamosi zitumike kwa ajili ya vikao vya Bunge

isipokuwa kwamba katika siku hizo Bunge litaanza saa tatu asubuhi hadi saa nane mchana na hakutakuwa na kipindi cha maswali kwa siku hizo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono na hoja hiyo inaendana na *supplementary Order Paper* ambayo inagawanywa hivi sasa, kwa shughui za leo, kwa hiyo naomba niwahoji sasa.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya shughuli hiyo, niwakumbushe tu Waheshimiwa Wabunge kwamba tunarudi hapa saa kumi kamili jioni ya leo na shughuli inayotuleta hapa ni uchaguzi wa Wabunge wa Afrika ya Mashariki.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maneno hayo, naomba nitishe shughuli za Bunge hadi saa kumi kamili leo jioni.

*(Saa 5.47 Asubuhi Bunge lilitishwa hadi saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tuwape nafasi Waheshimiwa walioko nje waweze kuingia ndani ili tuweze kuanza shughuli yetu jioni ya leo.

Waheshimiwa Wabunge, naamini muda wa kampeni umekwisha, kwa hiyo nawaomba sana kila mtu akae mahali pake ili tuweze kuendelea na shughuli yetu vinginevyo huku ni kuvuruga uchaguzi. Nawaomba sana ambao mko kwenye madawati ya watu wengine mrudi. Siyo vizuri nianze kuwataja majina nawaona wote.

Mheshimiwa Mbunge uliyepo kwa Mheshimiwa Mbowe nakuomba urudi kwenye kiti chako na Waheshimiwa wengine wote huko mlio kwenye maeneo yasiyo yenu nawaomba sana, wale walioko nje ya Ukumbi tunaomba muingie ndani zoezi hili kuna wakati lithitaji akidi, kwa hiyo nataka tuhesabiane tuwe na uhakika wa waliohudhuria ni wangapi.

Katibu!

**NDG. NENELWA M. WANKANGA – KATIBU MEZANI:**

**UCHAGUZI WA WABUNGE WA BUNGE LA  
AFRIKA MASHARIKI (EALA)**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nitaanza kwa utangulizi na naomba tusikilizane. Kama nilivyosema wale wanaotembea tembea naomba sasa watulie ili tuweze kwenda kwa kusikilizana. Waheshimiwa Wabunge wengine mbona hamkai chini? Kuna shida gani jamani? Mheshimiwa unataka kuongea kitu? Kuna shida gani leo?

Waheshimiwa Wabunge, uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Afrika ya Mashariki hufanyika kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 50(1)(2) ya Mkataba wa Kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki ambao umetiliwa nguvu na Sheria Na. 4 ya Mwaka 2001, *The Treaty for the Establishment of East African Community Act 2001 No. 4, 2001* na pia kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge.

Ibara ya 50 ya Mkataba wa Kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki umelipa Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mamlaka ya kupiga kura ili kuweza kuwachagua Wabunge tisa (9) watakaowakilisha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Bunge la Afrika ya Mashariki.

Kwa ajili ya kutekeleza jukumu hilo, Nyongeza ya Tatu ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, imeweka Kanuni *Rules of Procedure* ambazo zinaelekeza kuhusu masharti yanayopaswa kutimizwa na wagombea na

pia utaratibu unaotakiwa kufuatwa katika uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Afrika ya Mashariki. Ibara hiyo imeweka wigo wa uwakilishi katika Bunge la Afrika Mashariki *threshold*, kimakundi kama ifuatavyo:-

Kundi la kwanza ni *various political parties represented in the National Assembly*; kundi la pili ni *shades of opinion*; kundi la tatu *gender* na kundi la nne, *other special interest groups*. Kwa madhumuni ya kuwa na uwakilishi unaotakiwa kwa mujibu wa Ibara ya 50(1) ya mkataba huu na kwa kuzingatia mazingira ya Tanzania tukumbuke Wabunge hawa tisa pamoja na mambo mengine kila nchi inawachagua kwa kuangalia mazingira yao pia ilimradi wanatimiza vile vigezo vinne vilivyosemwa. Kwa hiyo, utaratibu wa nchi jirani unaweza kuwa tofauti na utaratibu wa Tanzania.

Kwa hiyo, katika utaratibu wa Tanzania, Kanuni ndogo ya 5 na Kanuni ya 11(3) ya Nyongeza ya Tatu ya Kanuni za Kudumu za Bunge zimeainisha uwakilishi huo kwa kuweka makundi yafuatayo:-

- (a) Wanawake
- (b) Zanzibar,
- (c) Upinzani na;
- (d) Tanzania Bara.

Upangaji wa makundi hayo umezingatia kwa kadri inavyowezekana wigo wa uwakilishi uliowekwa na Ibara ya 50(1) ya mkataba wa kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki, Kanuni ya 12 ya Kanuni za Kudumu za Bunge ongezeko la idadi ya Wabunge kwa Vyama vyenye uwakilishi Bungeni na mazingira ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Katika mgawanyo huo wa makundi nimegawa idadi ya wagombea kwa kila kundi chini ya Kanuni ya 11(4) ya Nyongeza ya Tatu ya Kanuni za Bunge. Upangaji huo wa idadi ya wagombea umezingatia uwiano wa idadi ya Wabunge waliopo Bungeni kwa kila Chama chenye uwakilishi Bungeni.

Hivyo, Spika ameamua idadi ya wawakilishi kwa kila kundi utakuwa kama ifuatavyo. Kundi (A), kutakuwa na Wabunge wawili kundi la wanawake, kundi (B), Wabunge wawili, Kundi (C) la Vyama vya Upinzani wao wana nafasi tatu kwa upande wao ambapo CCM kwa ujumla wake wana nafasi Sita (6) na kundi (D), Wabunge wawili. Hivyo idadi na uwiano wa Wabunge watakaochaguliwa kuiwakilisha Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki utakuwa kama nilivyoeleza hapo juu, kwa kurudia CCM Sita, CHADEMA wawili, CUF mmoja.

Baada ya maelezo hayo ya mwanzo, naomba sasa nimkaribishe Katibu wa Bunge ambaye ndiye *Returning Officer* ili naye aendelee kwa maelezo mengine ya ziada ya kuelekeza namna uchaguzi huu utakavyoendelea. Katibu tafadhali karibu.

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH – MSIMAMIZI WA UCHAGUZI:** Mheshimiwa Spika, naomba nitoe maelezo ya uteuzi wa wagombea Wajumbe wa Bunge la Afrika Mashariki na baada ya kuzingatia maelezo yako na uamuzi kwa mujibu wa Kanuni za Bunge. Awali ya yote niwashukuru sana wote ambao waliteuliwa katika Vyama vyao na kuwasilisha mapendekezo ya uteuzi, kugombea Ubunge wa Bunge la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, nilitoa taarifa kwa Vyombo vya Habari na nikathibitisha uteuzi wa Wagombea wa Chama cha Mapinduzi na nikasita kuridhia uteuzi wa wagombea wa Vyama vingine kutokana na upungufu mbalimbali ambao nilikiri kuwaandikia barua na nadiriki kusema kwamba vyama vimerejesha na vimetimiza masharti. Siyo dhamira yangu kueleza dosari zilizokuwepo, itoshe tu kusema kwamba nimeridhika na baadhi ya sababu zilizoainishwa lakini pia nimefanya uamuzi wa kuruhusu wagombea wa Vyama hivyo wawe wagombea. Nitaeleza baadaye.

Mheshimiwa Spika, tarehe 17 Machi nilitoa tangazo kwenye gazeti la Serikali Namba 376, kuhusu siku ya uteuzi na siku ya uchaguzi. Katika tangazo hilo nilipanga siku ya

tarehe 30 Machi saa 10.00 jioni kuwa siku ya uteuzi wa wagombea na siku ya tarehe 4 Aprili 2017 yaani leo, asubuhi kuwa siku ya uchaguzi lakini imefaa iwe saa 10.00 jioni kutokana na ratiba ya Bunge.

Baada ya hatua hiyo, Vyama mbalimbali viliwasilisha majina ya wagombea wapatao 20 kwa mchanganuo ufuatao. Chama cha Mapinduzi kiliwasilisha wagombea 12, CHADEMA wagombea wawili, Chama Cha Wananchi CUF nitaeleza baadae wagombea wanne, NCCCR mageuzi mgombea mmoja na ACT Wazalendo mgombea mmoja. Kati ya wagombea hao, wanaume ni 12 na wanawake ni 8, kwa mchanganuo ufuatao – CCM wanawake sita (6) na wanaume sita (6); CHADEMA wanawake hakuna, wanaume wawili; CUF mwanamke mmoja na wanaume watatu; nitalieleza hilo. NCCCR Mageuzi mwanamke mmoja na wanaume hakuna; ACT Wazalendo wanawake hakuna na mwanaume mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, majina hayo ya wagombea yaliwasilishwa na Vyama vyao tarehe 30 kabla ya saa 10.00 jioni kama masharti ya Kanuni ya 5 (4) Nyongeza ya Tatu ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2016. Baada ya hatua hiyo nilifanya uchambuzi wa nyaraka zilizowasilishwa ili kujiridhisha na uzingatiaji wa masharti ya uteuzi wa wagombea kwa mujibu wa Ibara ya 50 ya Mkataba, Ibara ya 67 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Sheria ya Uchaguzi wa Wajumbe wa Afrika Mashariki... *(Makofi)*

*(Hapa Mheshimiwa Peter A. Lijualikali aliingia Ukumbini baada ya kutokuwepo Bungeni kwa muda mrefu na Waheshimiwa Wabunge walimpigia makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane. Mheshimiwa Lijualikali karibu sana. Katibu tunaomba uendelee.

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH – MSIMAMIZI WA UCHAGUZI:** Mheshimiwa Spika, baada ya hatua hiyo ya mawasilisho ya Vyama, nilifanya uchambuzi wa nyaraka

zilizowasilishwa ili kujiridhisha na uzingatiaji wa masharti ya uteuzi wa wagombea kwa mujibu wa Ibara ya 50 ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Ibara ya 67 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Sheria ya Uchaguzi wa Wajumbe wa Bunge la Afrika Mashariki ya mwaka 2011, Masharti ya Kanuni ya Tano, Fasili ya (1), (2), na (3) ya Nyongeza ya Tatu ya Kanuni za Kudumu, Toleo la 2016.

Mheshimiwa Spika, ufuatao ni mchanganuo wa maombi ya wagombea katika makundi ya uchaguzi:-

Mheshimiwa Spika, walioomba kupitia Chama cha Mapinduzi katika Kundi (A) ni:- Ndugu Fancy Haji Nkuhi, Ndugu Happiness Elias Lugiko, Ndugu Happiness Ngoti Mgalula, Ndugu Zainab Rashid Mfaume Kawawa. Hili ni kundi la wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kundi (B) Zanzibar waliyoomba ni Dkt. Abdullah Hasnuu Makame, Ndugu Maryam Ussi Yahya, Ndugu Mohamed Yusuf Nuh na Ndugu Rabia Hamid Mohamedi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kundi (C) Vyama vya Upinzani, Ndugu Ezekiel Dibogo Wenje, Ndugu Lawrence Kego Masha, Ndugu Habibu Mohamed Mnyaa, Ndugu Sonia Jumaa Magogo, Ndugu Thomas Malima na Ndugu Twaha Issa Taslima. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, si nilisema kampeni zimekwisha? Katibu endelea.

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH - MSIMAMIZI WA UCHAGUZI:** Tanzania Bara kundi(D), Ndugu Adam Omari Kimbisa, Ndugu Anamringi Issay Macha, Ndugu Charles Makongoro Nyerere, Dkt. Ngwaru Jumanne Maghembe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wagombea ambao hawajakidhi masharti ya uteuzi, Vyama vya ACT- Wazalendo na NCCR- Mageuzi, viliwasilisha majina ya mgombea mmoja mmoja



kwa kila Chama. Chama cha ACT- Wazalendo kiliwasilisha jina la Profesa Kitila Mkumbo, wakati Chama cha NCCR - Mageuzi kiliwasilisha jina la Nderakindo Papetua Kessy. Baada ya kuzingatia masharti ya Ibara ya mkataba na Kanuni ya 12 ya Kanuni za Kudumu za Bunge na Mwongozo wa Spika kama alivyouainisha kuhusu uwiano na idadi ya kura zinazotakiwa kupigwa katika kila kundi, ilionekana kuwa vyama hivyo havina fursa ya kupata kiti katika uchaguzi huu. Uamuzi huu ulifikiwa baada ya kukokotoa uwiano wa Wabunge walilopo kama ulivyochoambuliwa katika Kamati ya Kanuni baada ya Mwakilishi wa Chama cha ACT kuomba tafsiri ya Kanuni, naomba hilo nisilirejee tena.

Mheshimiwa Spika, kutokana na matokeo ya uchambuzi na kwa kuzingatia masharti ya Ibara ya 50 ya mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kwa kuzingatia masharti ya Ibara ya 67 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa kuzingatia Sheria ya Uchaguzi wa Wajumbe wa Bunge la Afrika Mashariki Kanuni ya 12 ya Kanuni za Kudumu za Bunge na Kanuni ya 5 (1), (2), (3) ya Nyongeza ya Tatu ya Kanuni za Kudumu za Bunge na Mwongozo wa Spika kuhusu mgawanyo wa kura zinazotakiwa kupigwa katika kila kundi, kwa mamlaka niliyopewa kama Msimamizi wa Uchaguzi nilitoa taarifa na narejea kutoa taarifa kuwa wafuatao ndiyo waliokidhi vigezo na masharti ya kuteuliwa kugombea uchaguzi wa Wajumbe wa Bunge la Afrika Mashariki uliopangwa kufanyika leo tarehe 4 kwa mchanganuo ufuatao:

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea na mchanganuo huo ni vizuri nikarejea nilichokisema awali. Nimefuta pingamizi zilizotolewa na Chama cha CUF ndani ya Chama cha CUF. Kulikuwa kuna mapingamizi mawili ya kundi moja kupinga kundi lingine, kundi moja liliwasilisha jina moja na kundi lingine liliwasilisha majina matatu.

Mheshimiwa Spika, siyo dhamira yetu kama wasimamizi wa taratibu kuingia katika mgogoro, taratibu za uchaguzi zilitaka wagombea watimize masharti ya Ibara 67 ambayo inataka wagombea wawe na sifa za

kuchaguliwa kuwa Wabunge. Moja ya sifa ni kuwa lazima awe ana Chama cha Siasa. Niliomba Tume ya Taifa ya Uchaguzi ili kama wagombea wamekidhi sifa hizo na Vyama viliwasilisha Tume ya Uchaguzi kwa barua ya tarehe 28 Machi, 2016 barua Na. EA/75/162/24/71, iliyoelekezwa kwa Katibu Mkuu Chama cha Wananchi CUF, S. L. P. 10979 Dar es Salaam, ambayo naomba ninukuu: "Uthibitisho wa wagombea Ubunge wa Bunge la Afrika Mashariki, tafadhali rejea barua yako kumbukumbu namba hiyo, Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika kikao chake cha tarehe 28 Machi, 2016 imepitia na kuchambua nyaraka za Ndugu Mohamed Habibu Mnyaa, Ndugu Thomas Malima, Ndugu Sonia Magogo na Ndugu Twaha Issa Taslima, wanaopendekezwa kugombea Ubunge wa Bunge la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi huo Tume imejiridhisha kuwa, orodha ya wanaopendekezwa wanazo sifa za kuwa Wabunge kwa mujibu wa Ibara ya 67 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kifungu cha 36 cha Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, barua imesainiwa na Mkurugenzi wa Uchaguzi, haya ndiyo mamlaka niliyoyatumia katika kuwapitisha wagombea wote nilioletewa. Nadhani makundi yanayohusika yamenisikia.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo sasa nisome wagombea waliopitishwa kwa ajili ya kugombea.

Mheshimiwa Spika, wanawake Ndugu Fancy Haji Nkuhi, Ndugu Happiness Elias Lugiko, Ndugu Happiness Ngoti Mgalula, Ndugu Zainabu Rashid Mfaume Kawawa, hili ni kundi (A) la wanawake, wako wanne wanatakiwa wawili.

Kundi B Zanzibar ni Ndugu Abdallah Husnuu Makame, Ndugu Maryam Ussi Yahya, Ndugu Mohamed Yusuf Nuh, Ndugu Rabia Hamid Mohamedi. Wagombea wako wanne nafasi zinazotakiwa ni mbili mmoja mwanamke, mmoja mwanaume. Hii ni kutimiza sharti la Sheria ya Uchaguzi wa Bunge la Afrika Mashariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Vyama vya Upinzani ni Ndugu Ezekiel Dibogo Wenje na Ndugu Lawrence Kego Masha. Hawa ni wa Chama cha CHADEMA. Nafasi za CHADEMA ni mbili wagombea wako wawili. Hili nitalieleza.

Mheshimiwa Spika, Chama cha CUF, nafasi iko moja wagombea wako wanne; Ndugu Habibu Mohamed Mnyaa, Ndugu Sonia Juma Magogo, Ndugu Thomas Malima na Ndugu Twaha Issa Taslima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Tanzania Bara nafasi ziko mbili wagombea wako wanne. Nitawataja Ndugu Adam Omari Kimbisa, Ndugu Anamringi Issay Macha, Ndugu Charles Makongoro Nyerere na Dkt. Ngwaru Jumanne Maghembe.

Mheshimiwa Spika, nimemaliza kutoa taarifa ya wagombea waliopitishwa ili Bunge lako Tukufu liweze kuingia kwenye mchakato wa kuwapigia kura. Narejesha kwako ili uweze kuendelea na taratibu za uchaguzi.

**SPIKA:** Ahsante sana Katibu kwa maelezo hayo. Sasa tunajiandaa kuendelea na utaratibu *unless* kwa hatua hiyo kuna ufafanuzi wowote au jambo lolote ambalo mngependa mimi au *Returning Officer* aweze kulifanya kwa hatua hii. Ni mmoja tu eeh? wawili, zaidi ya Mheshimiwa Mnyika nani mwingine, Katibu nitajie majina.

Kwanza ni Mheshimiwa John Mnyika, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, Mheshimiwa Katani A. Katani na Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali ni wanne. Ahsante sana.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Jaku.

**SPIKA:** Haya tuanze na Mheshimiwa Jaku.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nataka kuuliza tu hawa wagombea wetu wataoneshwa kwenye vyombo vya habari *live* ili wananchi wetu wapate kuwaona na kuwatambua?

**SPIKA:** Swali hilo nilijibu moja kwa moja. Kwanza kwa kuwatambulisha wageni maalum tulio nao leo, mabinti zetu kutoka Msalato Girls *School* naomba msimame hapo mlipo. Karibuni sana sana. (*Makofi*)

Hawa ni mabinti walio kwenye shule ya watoto wenye vipaji maalum iliyoko hapa hapa Dodoma. Kwa hiyo, mjue tu siyo kwamba tuko *live* ambayo nawathibitishia kwamba tuko *live* na Watanzania wanawaona lakini pia watoto wetu wapo wanawaona na wangependa kujifunza kutoka kwenu. Mheshimiwa Jaku nimekujibu tuendelee na Mheshimiwa Bobali. (*Makofi*)

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Spika nakushukuru. Nitaeleza machache ingawa nimeona *Chief Whip* amesimama ila nataka kujua juu ya utaratibu wa uendeshaji wa uchaguzi huu Chama cha *CUF* kipo kwenye mgogoro wa uongozi na suala hili liko Mahakamani na kwa kuweka rekodi sawa wiki iliyopita Mahakama imefanya maamuzi kwamba hata ruzuku ambayo inatolewa kwa Chama cha *CUF*, hivi sasa imezuiwa isipelekwe kwa upande unaoitwa wa Lipumba na wala isipelekwe kwa upande huo unaoitwa upande wa Maalim Seif. Mahakama chini ya Jaji Dyansobela imefanya maamuzi ya namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, pia sielewi labda Msimamizi wa Uchaguzi atufafanulie kwamba kama Kanuni zinaruhusu wagombea wa kiti kimoja kuwa wanne kutoka kwenye Chama kimoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu kesi iko Mahakamani kama kesho Mahakama itaamua kwamba Lipumba siyo tena Mwenyekiti na ameleta wagombea ambao leo tunakwenda kuwachagua kuwa Wabunge wa Afrika Mashariki, hatuoni kwamba Chama cha *CUF* kitakuwa hakijatendewa haki kwa sababu mgombea aliyepitishwa atakuwa amepitishwa na mamlaka ambayo siyo halali ndani ya chama. Kwa hiyo naomba ufafanuzi.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Spika, naomba ufafanuzi na sisi tulifarijika tulipopata barua ya leo kwamba haijateua mgombea kutoka Chama cha *CUF* lakini sijui kumetokea nini kwamba ndani ya masaa mawili mnabadilisha maamuzi ya haraka, naomba mwongozo wako.

**SPIKA:** Ahsante sana muda hauko upande wetu. Kabla hujakaa je, Mahakama ikiamua kwamba wale waliioletwa upande wa Mheshimiwa Maalim Seif hawana haki, kwa hiyo hoja yako ni kwamba....

*(Hapa Wabunge fulani waliongea bila mpangilio kutokana na kauli ya Mheshimiwa Spika)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, ulipokuwa unaongea nilikusikiliza mbona mimi unanitupia mikono namna hiyo? ndiyo utaratibu huo, tuheshimiane. Unapotoa hoja hapa ni mahali pa watu wazima nimesema nchi nzima inatuangalia, wewe unatoa mfano wa wenzio, Mahakama hiyo ikiamua vinginevyo? Kwa hiyo, mambo ya Mahakama tuiachie Mahakama, hapa hatujadili ruzuku wala kitu gani mambo ya Bunge mwachieni Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mnyika halafu Mheshimiwa Katani.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Uchaguzi huu unapaswa kuendeshwa kwa mujibu wa Kanuni na moja ya Kanuni ya msingi, ambayo wewe umeizungumza na msimamizi ameizungumza ni Nyongeza ya Tatu ya Kanuni. Ambayo katika Kanuni ya 5(5) inasema *“any political party which is entitled to sponsor candidates may submit to the Returning Officer the names of three candidates for each vacant seat in the following relevant groups”* *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa tafsiri nyepesi tu ni kwamba kila chama kinachotaka kuleta mgombea kinaweza kuleta majina yasiyozidi matatu kwa kila nafasi inayogombewa. Sasa Msimamizi wa Uchaguzi muda mfupi

uliopita ametangaza uteuzi wa wagombea ambapo kwenye kundi la Upinzani katika kiti alichosema ni kimoja kinachogombewa na Chama cha Wananchi CUF amesema wameteuliwa wagombea wanne.

**SPIKA:** Wakati mnachagua Wabunge wa Mabunge haya mengine ambayo Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani kwa heshima kubwa ameya-*refer* hapa, kwa kweli mimi nilikuwa hospitali, kwa hiyo, siwezi kukumbuka *exactly* mlichokifanya. Utaratibu ni kwamba japo sikuwepo, hao mliowapitisha siku hiyo, Bunge hili lililojiwa. Ndiyo ninyi mkasema sawa waende. (Makofi)

Hakuna wakati wowote ambapo wamewahi kuletwa watu hapa halafu wakapita moja kwa moja tu kwamba wamepita. Sasa *role* ya Bunge ni nini? Kwa nini wamekuja hapa sasa? Wamekuja kufanya nini sasa? Unapigiaje kura mtu ambaye amepita bila kupingwa? (*Kicheko*)

Kwa hiyo, kura ya wale kiutaratibu inakuwa kama tulivyofanya kwa wale wengine, ndiyo utaratibu wetu wa Kibunge.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, naomba tena nafasi tafadhali.

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako, naomba nirudie tena kwa Bunge hili. Sheria inayosimamia uchaguzi wa Wabunge wa Afrika Mashariki iko *very specific*, kura ni za siri. Haitoi *provision* ya kupiga kura za wazi. Sheria ipo na imesema.

Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, nashauri tuwe tunasoma sheria kabla ya kuanza kubishana humu ndani. Tuwe tunasoma na hizi kanuni tuelewe zinaelekeza vipi. Kwa mambo ambayo tunatumia utamaduni na maelekezo ya Spika, ni pale ambapo kuna maeneo ambayo hayana maelekezo sahihi ya kisheria na kikanuni. Sasa hili jambo liko wazi sana na sijui wenzetu wa upande wa pili mna hofu ya nini?

Mheshimiwa Spika, kwa kuhoji ni kura ya wazi na siyo kura ya siri.

**SPIKA:** Kwa hiyo, unachopendekeza Kiongozi wa Upinzani kwa hawa wagombea wako tunawachaguaje? Bunge hili linawachagua kwa utaratibu gani?

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, wagombea ambao wako kwenye *ballot paper* na ambao hawana mpinzani, tafsiri yake ni kwamba watakuwa ni

wagombea waliopita bila kupingwa. Kwa sababu...  
(Kicheko)

**SPIKA:** Naomba Kiongozi wa Upinzani nipe kanuni inayosema hivyo, kwamba huyo anapita bila kupingwa. Kanuni ipi? (Makofi)

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Lete hiyo *Article 11* hiyo, ngojeni.

**MBUNGE FULANI:** Vyeti, vyeti, acha maneno.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, utaratibu umeandikwa kwenye Kanuni, lete ile Kanuni Mheshimiwa Lissu.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbowe wakati nakupa muda utafutetafute hapo, hebu tusikilize kuhusu utaratibu.

### KUHUSU UTARATIBU

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Spika, nilitaka kusema, wakati anatusomea hiyo kanuni, pia aangalie ni kwa nini chama cha upinzani hakikuleta wanawake?

**MBUNGE FULANI:** Wewe zero wewe, kaa kimya wewe.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Spika, kama mnazingatia kanuni, pia suala la *gender* lizingatiwe. Kwa hiyo, haijawahi kutokea mnakwenda kupitisha viongozi bila kuhojiwa. Sasa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani unaogopa nini? Sasa tupe utaratibu unaotaka kusema, lakini atuambie mbona hakuna wanawake?

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika,...

**SPIKA:** Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani endelea.



**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, niko tayari. Kwa faida ya Waheshimiwa Wabunge kadhaa ambao wanauliza hoja ya *gender*, niwape ufafanuzi ili nifunge mjadala huo.

Waheshimiwa Wabunge, *Treaty* ya Afrika Mashariki inahitaji Wabunge tisa na masharti yanasema kwamba katika hao tisa, angalau theluthi moja wawe ni *either gender*. Ambacho *treaty* hajasema, halijasema *process* nzima itawaliwe na utaratibu huo, ila utaratibu wa nchi na ile *delegation* ya nchi, yaani *end product* mwisho wa siku ndiyo *i-reflect* theluthi moja.

Mheshimiwa Spika, kwa utamaduni na utaratibu uliopangwa, labda niwafahamishe maana wengine hamwelewi, msikilize basi.

Kwa utaratibu ambao ulipangwa na uongozi wa Bunge yalikuwa ni makubaliano kwamba kutokana na mgawanyo wa viti kwa vyama mbalimbali, kwa mfano Chama cha Wananchi (CUF) kina nafasi moja...

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Taarifa Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani. Mheshimiwa Mama Nagu nimekusikia.

#### TAARIFA

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kutoa taarifa.

*(Hapa microphone ilikata sauti)*

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mnanifanyia fujo ninyi!

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Halima anawasha hiyo *microphone*, tunakuona.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Spika, nimesikia alichosema Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kwamba kwa masharti ya Afrika Mashariki wana theluthi moja. Nataka nimpe taarifa kwamba namba ya chini, theluthi moja...

*(Hapa microphone ilikata sauti)*

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Spika, hiyo ndiyo taarifa ambayo nataka kuwapa.

**SPIKA:** Jaribu kutumia *microphone* ya jirani pale tuone. Tumia ile ya jirani.

Kuna mchezo unachezwa hasa upande huu, ndiyo *record* niliyopata. Mkumbuke haya mambo ni *computerized*. Kwa hiyo, ni rahisi sana kujua, kwa sababu kila wakiongea Wabunge wa upande huu *microphone* zinakataa. Mkiongea ninyi *microphone* zinafanya kazi. Ni michezo ya kitoto. Muwe na hali ya kuweza kusikiliza wenzenu. Shida yenu nini? Mbona ninyi mkiongea wenzenu wanawasikiliza? Kwa nini tunakuwa hivyo lakini? Litakuwa ni Bunge la aina gani la watu ambao wanataka kuongea wenyewe peke yao tu? *(Kicheko)*

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Spika, nilichotaka kusema ni kwamba hiyo theluthi moja ni idadi ya chini kabisa lakini inaweza kuwa zaidi. Kwa maana hiyo, kila chama kinapaswa kiwe kimeeleza hilo, siyo kingojee vyama vingine peke yake vitekeleze. Kwa hiyo, kwa kweli na CHADEMA wanawajibika kuzingatia *gender* zote mbili.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Kuhusu Utaratibu.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika,...

**SPIKA:** Kidogo tu, kabla Kiongozi wa Upinzani hujaendelea, nasikia sauti ya Halima Mdee anapinga wanawake wa CHADEMA wasigombe. Haya nakupa nafasi.

**MBUNGE FULANI:** Wallopinga wale...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, hizi ndizo tunaita *cheap politics* bila kuwa na ...

Mheshimiwa Spika, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni alikuwa anataka kuwapa elimu ya *Treaty* na Sheria ya Uchaguzi ya Mabunge ya *EALA* inasema nini kuhusiana na zile nafasi tisa na suala la jinsia zote mbili zisipungue moja ya tatu. Kwa hiyo, inaweza ikawa jinsi ya kike ama jinsi ya kiume. Sasa nashangaa watu mnasimama hapa mna-*propagate* vitu ambavyo havina ukweli.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, CUF ina nafasi moja. Hivi hiyo nafasi moja, *one third* inatoka wapi?

**MBUNGE FULANI:** Watuambie.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, CHADEMA ina nafasi mbili, hivi kwenye nafasi mbili *one third* inatoka wapi? CCM mna nafasi sita, katika hizo nafasi sita *one third* ipo.

Kwa hiyo, ndiyo maana kutokana na huo ukubwa na mfumo wetu wa kikanuni, naomba tusikilizane, tunawapa shule. Tatizo hamsomi. *Treaty* na Sheria ya Uchaguzi wa Afrika Mashariki inasema *elected members*. Tunaangalia *elected members*, hatuungalii wagombea. Kwa hiyo, tunatakiwa kama nchi tuangalie baada ya uchaguzi huu...

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Halima, ahsante sana muda wako umeisha.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, baada ya uchaguzi huu... nawaelemisha hawa hawaelewi wanarukaruka tu.

**SPIKA:** Unaowaelemisha walikuwa wanakuuliza tu katika wagombea wako wale wanaume wawili, mwanamke nani pale? (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Ninachosema ni hivi...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Subiri nimalize basi, wewe niambie, ukiniambia *one third* ya ...

**SPIKA:** Tayari Mheshimiwa Halima. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, endelea.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge watakumbuka asubuhi Msimamizi wa Uchaguzi alitusomea maelezo marefu hapa ndani ya Bunge hili Tukufu na akatueleza kuhusiana na baadhi ya vyama vya siasa, ambacho amesisitiza ni sharti...

*(Hapa microphone ilikata sauti)*

**SPIKA:** Watu wa *IT* na watumishi wa Bunge, pigeni jicho mniambie anayefanya ukorofi huu ni nani?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu Msimamizi wa Uchaguzi wajibu wake ni kutoa mwongozo wa kisheria, lakini yeye hachagui, hawalazimishi Wabunge. Ndiyo maana, hilo suala la kisheria anahoji sasa...

*(Hapa microphone ilikata sauti)*

**SPIKA:** Mheshimiwa nakuomba uje mbele hapa, *microphone* zinasumbua sana leo.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, tutakumbuka wote asubuhi, Msimamizi wa Uchaguzi na Kanuni hizi zinamtambua Katibu wa Bunge kwamba ndiye Msimamizi wa Uchaguzi na kwamba uchaguzi huu utasimamiwa na kuendeshwa na Msimamizi wa Uchaguzi ambaye ni Katibu na asubuhi ametueleza maelezo mbalimbali ambayo yanahusiana na baadhi ya vyama kushindwa kukidhi masharti ya uchaguzi...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mchana ulisemaje? Tuongoze kwenye Kanuni bwana, acha porojo.

**MBUNGE FULANI:** Mchana si walibadilisha lakini, ninyi mna-*withdraw*...

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kura zinapigwa na Waheshimiwa Wabunge, naye kama Msimamizi wa Uchaguzi hataki kulielekeza Bunge lifanye kitu ambacho anaona ni uvunjifu wa sheria. Kwa hiyo, wakati wa kupiga kura ndiyo kunaletwa huo umuhimu wa kuwahoji Waheshimiwa Wabunge, kusudi...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Taarifa. Soma Kanuni bwana, usitupotezee muda hapa.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Kanuni ziko wazi ndiyo, lakini kuna hilo suala la wajibu wa kisheria, ndiyo msingi. Sasa je, Wabunge wakubali wao wenyewe wavunje sheria au wasivunje sheria?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Sheria ipi?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, huo ndiyo msingi wa kuhojiwa.

Mheshimiwa Spika, kwenye hili nilikuwa nashauri kwamba Wabunge msiahirishe uchaguzi huu. Tusiahirishe uchaguzi na kwa sababu hata kwa mujibu wa Kanuni hakuna kuahirisha uchaguzi. Kwa hiyo, wapige kura leo hii. Ndiyo ushauri wangu.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Aliyekwambia tunaahirisha nani?

**SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, aliyekuwa anaongea alikuwa ni Mheshimiwa Mbowe, namrudishia atupe kile kipengele cha kupita bila kupingwa.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, hoja ni ya kwangu naomba nielekeze ninavyotaka kuielekeza.

Mheshimiwa Spika, nimesema kwamba uchaguzi wa Wabunge wa Afrika Mashariki unasimamiwa na sheria ambazo ziko *very specific* na ndiyo naomba nizisome. *Article (5)* inasema: "*Any political party which is entitled to sponsor candidates may submit to the Returning Officer the names of the three candidates for each vacant seat in the following relevant groups.*"

Sasa wote tunatunga Sheria hapa, tukishasema "*may*" chama kinaweza kikaleta mgombea mmoja, wawili au watatu. Hii ndiyo *consensus* ambayo tumeifikia kwenye Kamati ya Kanuni, wala ilikuwa haina ubishi. Naomba tuelewane hapa, Chama cha Mapinduzi kilipoleta wagombea wawili, hakuna mtu aliyepinga.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbowe, samahani tu kidogo.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Naweka msingi Mheshimiwa Spika. Naomba tafadhali...

**SPIKA:** Kidogo tu...

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Ndiyo.

**SPIKA:** Tulipokuwa tumefika palikuwa mahali pazuri tu pa hoja yako kwamba Wagombea wako wapite bila kupingwa. Ndiyo tukasema tupe tu Kanuni ili tu...

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, nakwenda huko, lakini kwa sababu kuna hoja zimejitokeza hapa kwamba mmeleta mgombea mmoja, nafafanua ili tuwekane sawa hapa kwenye misingi, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukakubaliana mtu unaweza ukaleta mgombea mmoja, unaweza kuleta wagombea wawili na wengine wameleta wagombea

watatu. Nikirudi sasa kwenye kifungu kinachohusiana na uchaguzi na upigaji kura ambacho ni *section 11*, Mheshimiwa Lissu alikisoma, kwa sababu mlikuwa hamumsikilizi naomba nikisome tena ili tujue kwamba uchaguzi wa Afrika Mashariki una maelekezo.

Mheshimiwa Spika, nikianza na 11 yenyewe; *"The voting shall be conducted under the general supervision of the Returning Office."* Hii hatuna *dispute*. *Article 11(2): "The Returning Officer shall issue only one ballot paper to each voter."*

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya ambayo tunayo sasa hivi, hata hiyo *ballot paper* hatujawahi kuoneshwa *sample* yake, hatuijui. Kwa hiyo, pengine tunabishana kitu ambacho tukiruhusiana tupeane *ballot paper* tukaridhika kwamba hiyo *ballot paper* moja inakidhi wagombea wote tutakuwa tume-*make progress*, hilo la pili.

Mheshimiwa Spika, *11(3) "The ballot paper shall contain the names of all candidates arranged alphabetically in the following groups:-*

*Group A: Women Candidates;*

*Group B: Zanzibar Candidates;*

*Group C: Opposition Parties Candidates; and*

*Group D: Mainland Candidates.*

*11(4) A voter shall be required to cast a specified number of votes to be announced by the Speaker in each of the groups.*

*11(5) On receiving a ballot paper, each voter shall secretly record his votes by putting a mark against the names of the nine candidates he wishes to vote for." (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *ballot paper* iko pale, ina wagombea wote. Nikisoma kifungu kidogo cha (6), na msikilize vizuri. Kifungu cha 11(6) *"Each voter shall be required to cast as many votes as there are vacancies, otherwise his whole ballot paper will be regarded as spoilt."*

Mheshimiwa Spika, hapa ndipo ninapokuja kwenye hoja yangu ya msingi. *Ballot paper* ipo, inatakiwa majina tisa. Ukipigia Wagombea nane, *ballot paper* imeharibika na sheria inasema hivyo. Kwa hiyo, sheria haijasema mahali popote pa kuhojiana; inakuja *ballot paper*, ina majina ya Wagombea wote, lazima uchague watu tisa kutoka makundi yote...

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Taarifa Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Kidogo tu Mheshimiwa ili amalize, lakini nitaipokea moja kwa moja usiwe na wasiwasi.

Mheshimiwa Mbowe, ninachotaka, umalizie tu kwa kutuambia sasa katika kuchagua hawa *candidates* wako, Wabunge wangu hawa watachaguaje kama sawa au siyo sawa?

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Sasa nafasi iko hapo, unatakiwa upige kura tisa, pigia kura hapo.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa!

**SPIKA:** Kwa maana ya kura ya ndiyo na hapana au kwa maana gani yaani? Kuwa wazi, maana ulisema wagombea wako wanapita bila kupingwa, nawe mwenyewe unanza kujipinga tena kwa kusema kwamba lazima mtu apige kura tisa. Sasa walishapita bila kupingwa, unapigaje kura tisa tena?

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, wewe mwenyewe Spika unajua katika *general practice* za uchaguzi katika nchi yetu popote zilipo, mgombea anapokuwa hana mpinzani anapita bila kupingwa. Tunachosema, kwenye sheria hizi lazima m-*tick* pale kwamba kapita. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, nimekuona, Taarifa. Halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Simbachawene. Kingwangalla kwanza.



## TAARIFA

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ...

*(Hapa microphone ilikata sauti)*

**SPIKA:** Yuko mtu anayecheza cheza na hizi *microphone*, karibu nampata sasa hivi. Nimeshapewa majina yake mara mbili, tatu, nataka tu ku-*confirm*, halafu basi tumu-*embarrass* mbele ya nchi nzima kwamba amekataa kujiheshimu. Endelea Mheshimiwa Kigwangalla.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, hizi Kanuni zimeandikwa, na mimi nimepata bahati ya kuwa nayo, nasoma mle mle ambamo Mheshimiwa ananukuu... kwa mfano... kwenye Kanuni namba tano ambayo... inasomeka kama ifuatavyo; *"A political party ... sponsor candidates... the names of..."*

*(Hapa microphone ilikata sauti)*

**SPIKA:** Njoo utumie *microphone* hii ya mbele hapa.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, ukisoma Kanuni ya Tano ambayo Mheshimiwa Mbowe na hata Mheshimiwa Lissu ameinukuu hapa, inasomeka kama ifuatavyo: *"Any political party which is entitled to sponsor candidates, may submit to the Returning Officer the names of three candidates for each vacant seat in the following relevant groups: the names of three candidates."* Pigia mstari hapo, majina ya wagombea watatu, *in each of the vacant seat in the following relevant groups.*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Subirini basi, nasoma tena. Mbona sisi tunakuwa wastaarabu na tunawasikiliza! Tujenge hoja kama tumeenda shule, siyo kupiga kelele.

Mheshimiwa Spika, tukienda mbele Kanuni ya 11...

**MBUNGE FULANI:** Soma kwa Kiswahili Mheshimiwa Kigwangalla.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, kanuni ya 11(4) inasomeka; *“A voter shall be required to cast a specified number of votes to be announced by the Speaker in each of the groups.” To be announced by the Speaker, napigia mstari hapo, kwamba Spika kwa kila kundi ambalo limewekwa hapa katika yale makundi manne ana mamlaka kwa mujibu wa Kanuni hii kutangaza kura ngapi zipigwe, in each; inasema tu simple, kwamba “A voter shall be required to cast a specified number of votes to be announced by the Speaker in each of the groups.”*

Kwa hiyo, Spika ametutangazia hapa tupige kura ngapi kwenye kila kundi. Sasa naomba Mheshimiwa Mbowe aichukue taarifa hii, kama na hii Kanuni pia ameisoma ama hakuisoma na kwamba mamlaka ya Spika ni nini kwenye hili halafu atupe ufafanuzi.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa!

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Mbowe atuoneshe Kanuni ambayo inaelezea *in case* kuna Mgombea ambaye hajapingwa na Mgombea mwingine, nini kifanyike. Maana nime-*peruse* hiki kitabu mwanzo mpaka mwisho, sijaona Kanuni hata moja ambayo inasema kama kuna nafasi moja na kuna Mgombea mmoja, nini kifanyike.

Ninaomba atuoneshe hiyo Kanuni kama anayo ili tuelewe, pengine tunaweza tukamuunga mkono. Kama hakuna, tusipotezeane muda, tufuate busara ya Spika kama ambavyo Kanuni ya (5) inatueleza humu ndani.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. PENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Simbachawene na wewe uje hapa mbele. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, nimemsikiliza Mheshimiwa Mbowe kwa makini sana. Amejaribu kueleza, lakini mwanzo alikuwa hafiki kwenye *conclusion*, mara ya mwisho akafika kwenye *conclusion*.

*I am George Simbachawene.* Alikuwa hafiki, lakini mara ya mwisho akafika kwenye *conclusion*, kwamba wao kwa kuleta *fixed number* ya wagombea ni kwamba wamepita bila kupingwa.

Mheshimiwa Spika, shida unayoipata ni je, Bunge hili limekuja kupiga kura au limekuja kuwatazama tu wagombea? Maana tuelewane, *that is the bottom line*. Bunge hili limekuja kuwachagua wagombea na utaratibu umeelezwa katika Kanuni ya 11 na Mheshimiwa Mbowe umeisoma vizuri sana. Hiyo unayoisema haipo kwenye Kanuni hii, *the word "may" katika sheria, if you give it a legal construction*, siyo tu inakupa uhuru wa kuamua, bali huwa inatatua matatizo yanayoweza kujitokeza ili uweze kupanga utaratibu unao-*fit* mazingira ya wakati huo. Hata ukitikisa kichwa lakini kasome vitabu, nakwambia.

**MBUNGE FULANI:** Hapo umechapia!

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, neno "*may*" linatujengea mazingira sasa ya kumaliza tatizo hili waliloleta wenzetu kwamba badala ya kutetea wagombea ili tuchague, wametuletea *fixed number*.

Sasa hatuna *option* nyingine. Tuliyonayo hapa ni Bunge lazima lipige kura kwenye hilo kundi; kwenye makundi mengine tunaweza tukapiga kura kwa sababu tuna *choice*, kwenye kundi hili hatuna *choice* zaidi ya kutumia neno 'Ndiyo' na 'Hapana.' Kwa hiyo, ni lazima tuhojiwe. (*Makofi*)

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, hauna *option* nyingine, ni lazima tuhojiwe ili hilo kundi liwe limepigwiwa kura.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu!

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, usipohoji na Wabunge wakasema ‘Ndiyo’ au ‘Hapana,’ maana yake ni kwamba kundi hilo halijapigiwa kura. Maana yake nini? Maana yake ni kwamba kura imepigwa huko, hapa hatupigi kura, nasi tumekuja hapa kuwapigia kura Wabunge wa *EALA*.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, Taarifa!

**SPIKA:** Kuna Mbunge amesimama muda mrefu sana kule. Ni Mbunge wenu pia, hebu tumsikilize, amesimama masaa mengi sana. Nakupa nafasi ndugu yangu.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, na mimi unione baadaye! Lusinde hapa.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nimesimama, lakini naomba niseme kwamba katika maelezo ya awali aliyoyasema Mheshimiwa Simbachawene, anapozungumza habari ya kusema kura za kuitikia ‘Ndiyo’ au ‘Hapana,’ hata Kanuni zetu hazitaji mahali ambapo katika kura hizi za *East Africa* kuna kuhoji Wabunge pale ambapo kuna Mbunge ambaye hana mpinzani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama maelekezo ya Kiti chako siku za nyuma kwamba pale ambapo hakuna Kanuni au Kanuni zimekaa kimya kuhusu jambo fulani, inatumika utaratibu wa Kibunge wa Mabunge mbalimbali katika kushughulikia jambo hili hapa. Hoja tulizozileta hapa, kuna hiyo hoja ya kuitika ‘Ndiyo’ au ‘Hapana’ ambayo haipo. Sasa inaonekana tumehama kwenye hoja ambazo tumeshatoa

*ruling* kuhusu *candidates*, tunaanza kurudisha mjadala katika mambo ya msingi ambayo tulishayaamua kwamba walioletwa tayari wame-*qualify*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Kiti chako kitumie busara ka sababu inaonekana kuna hujuma zinatakiwa kufanyika hapa kuhusu upande wetu wa upinzani. Kama Kiti chako kitatenda haki, basi usimamie katika haki.

**SPIKA:** Nakuomba ukae. Nilidhani kwa mtu yeyote mwenye nia njema, unasimama tu unasema ninachopendekeza utaratibu ambao naona utumike ni huu. Ukianza kusema maneno ambayo hayapo, nadhani haitusaidii hata kidogo. Mnasimama kumbe hata hoja yenyewe hamna.

Wewe una-*dispute* lile pendekezo ambalo nililitoa. Si uweke *alternative*. *Alternative* yako ni nini? Uwe *backed* na Kanuni, uchukue dakika moja, tunasonga mbele. Siyo unasimama, ooh, njama, njama. Njama iko wapi? Una ushahidi nayo? Kwa hiyo, wewe unapopinga hili, sema badala yake nini? Ndiyo mtu mzima anavyofanya.

Hawa wagombea wawili kwenye *ballot paper*, mimi nina *ballot paper* za aina tofauti za kila aina. Kwa utaratibu niliosema ambao ni *standard* kwa *Commonwealth*, kwa majina ya aina hii Spika anawahoji, wenyewe mnaamua. Sasa mnasimama mnasema aah, tunadhani utaratibu huo Mheshimiwa Spika hapo umekosea. Utaratibu mzuri ni huu kwa mazingira yetu. Mnaongea, utaratibu hamwoneshi. Mnasema tu wamepita bila kupingwa. Hiyo haiwezekani, haipo. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kama mlikuwa na mawazo hayo yafuteni kwanza, sasa wazeni upya. Usiwe kama jiwe, yaani ukishakamata jiwe, basi pale pale tu. Hakuna habari ya kupita bila kupingwa, haipo. Kwa hiyo, sasa tunafanyaje katika mazingira haya?

Mheshimiwa Pendo!

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, hapa. Halafu hapa kwa Lusinde.

**SPIKA:** Mheshimiwa Peneza ongea.

**MHE. PENDO F. PENEZA:** *Chief Whip.*

**SPIKA:** Hakuna cha *Chief Whip!* Mnasimama wote, namwita ambaye amesimama. Sasa, usisimame tena. Usinisumbue tena Mheshimiwa Pendo eeh! Maana mnanisumbua ninyi.

Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu! Mheshimiwa Mhagama, hujaongea.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika...

*(Hapa microphone ilikata sauti)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Jenista, tafadhali.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, naomba niseme mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza, nilichoridhika ni kwamba wote tunakubaliana na nimemsikiliza Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni na Wabunge wote waliochangia, kwanza wote tunakubaliana kwamba kwa mujibu wa *East African Treaty* ni kwamba uchaguzi huu ni lazima Wagombea wote wapigiwe kura, hilo wote tunakubaliana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama tunakubaliana wote wapigiwe kura, Kanuni zetu, kwanza ile Kanuni ya 11 inampa mamlaka *Returning Officer.*

**SPIKA:** Kwa hatua hiyo Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa wote wanapigiwa kura, neno kupita bila kupingwa halipo. Tunaendelea.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, hilo halipo. Nadhani hilo wote tumekubaliana kwamba hakuna atakayepita bila kupingwa kwa sababu ukiangalia *East African Treaty* na Kanuni tulizonazo; na ninashukuru sana hata Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni ametusaidia hilo kwamba ni lazima wagombea wapigiwe kura. Kwa hiyo, hilo wote tunakubaliana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa ni lazima hapa tutoke tuanze kuchukua utaratibu wa kuwapigia kura wagombea wetu. Kama tunaona kwamba hizi *procedures* zote tulizojiandaa mpaka hapa zimetufikisha mahali hatuwezi kwenda mbele, nilichokuwa nataka kushauri; lengo letu sisi tupate wagombea wote tisa watakaowakilisha makundi yote.

Mheshimiwa Spika, kama tumegundua kwamba kuna eneo ambalo linatupa shida, kifungu cha 17 kinakupa wewe mamlaka ya kutuongoza tunafanya nini. Kinakupa wewe mamlaka ya kutuongoza, tufanye nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama hivyo ndivyo, sioni kwa nini hapa tunaendelea kubishana tu. Tupewe maelekezo, kwanza karatasi yetu ya kura inafananaje? Tukishajua karatasi yetu ya kura inafananaje, tufanye maamuzi hapa. Kwanza ni lazima tukubaliane hakuna mgombea tutakayempitisha bila kupingwa...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Taarifa!

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, ni lazima kila mgombea apigiwe kura. Sasa karatasi yetu sisi ya kura ituongoze hapa kitu cha kufanya kiasi kwamba tutekeleze wajibu wetu wa kumpigia kila mgombea kura na hatutaweza kupitisha mgombea hapa bila kupinga.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 79(1) inatoa pia mwongozo wa utaratibu ambao tunaweza kuutumia kupiga kura kwa namna ile ambayo wewe kwa Kanuni ya 11 ambayo inampa mamlaka *Returning Officer* wetu, ana uwezo pia wa kutusaidia kujua tunafanya nini.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa natoa ushauri huo, tutoke tuendeleo na kazi, tusiendeleo kubishana. Hapa tutabishana mpaka asubuhi na hatutaweza kumaliza.

**SPIKA:** *Returning Officer.*

**MBUNGE FULANI:** *Ballot paper.*

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH – MSIMAMIZI WA UCHAGUZI:** Mheshimiwa Spika, naomba niwarejeshe. Bahati mbaya sana wakati nazungumza sikupata fursa ya kufanya uchambuzi.

Kwanza nikiri kwamba Kanuni ya 12 nafikiri wengi mnaiona, inasema uchaguzi wa Wabunge wa Afrika Mashariki na kwamba Wabunge wa Bunge hili mtapaswa kuwachagua, nime-*underline* maneno.

Mheshimiwa Spika, sasa kuchagua ina tafsiri pana, inaanzia katika vyama. Kuna uchaguzi. Jambo hili lilijadiliwa kwenye Kamati ya Kanuni vizuri zaidi. Sasa Bunge linapoletewa jambo lolote kwa sababu, jambo linalokuja Bungeni ni lazima lije kwa hoja au kwa ombi au kwa taarifa ambayo Bunge litaipokea na kufanya maamuzi, huo ndiyo utaratibu wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, niliomba niwarejeshe katika msingi mzima wa maamuzi ya Bunge. Bunge linaamua katika njia tatu; kwanza, kama jambo limewekewa utaratibu wa uamuzi kanuni inayohusika ndiyo inayotumika. Kwa hiyo, nirejee ya Kiongozi wa Upinzani, amezungumza vizuri.

Mheshimiwa Spika, katika Nyongeza ya Tatu, uamuzi wa wagombea wanaopita bila kupingwa haujaainishwa. Nataka niseme wazi, tunaogelea wote, haupo. Hata kama hawakupita bila kupingwa, endapo kungekuwa kuna wagombea watatu wakafungamana, Kanuni haziweki wazi, zimempa Spika mamlaka kwenye fasili ya 17 kuzingatia, kwanza taratibu na kanuni nyingine zinazosimamia uchaguzi ndani ya Kanuni za Bunge. Soma Kanuni ya 12 inasema



uchaguzi utazingatia Kanuni za Bunge. Mamlaka yote ya Spika anatafsiri kanuni zote *harmoniously*, haizungumzii kanuni moja.

Mheshimiwa Spika, tunakwenda Kanuni ya 79, Bunge linaamua kwa namna tatu. Kwanza yale yanayohitaji kuamuliwa kama kuna Kanuni, yataamuliwa; yale ambayo hayapo, Bunge litaamua. Naomba niisome; "Kwa Wabunge kufuata maoni ya walio wengi, waliohudhuria na kupiga kura." Ya pili, "Eendapo mambo hayakuwekewa utaratibu Kanuni ya 79, Fasili ya (4), "isipokuwa kama imeelekezwa vinginevyo."

Mheshimiwa Spika, naomba nirejee, katika Kanuni hizi uamuzi juu ya mambo yote utapatikana kwa kufuata wingi wa sauti za Waheshimiwa Wabunge za 'Ndiyo' au 'Siyo' na Spika atatangaza matokeo ya kura. Inakwenda zaidi inasema: "Endapo Mbunge hatoridhika na sauti, ataomba kura zipigwe."

Mheshimiwa Spika, sasa ninachotaka kusema, sioni kwa sababu gani Bunge lako Tukufu liende mbali katika kufikia uamuzi, kanuni zimetupa jibu. Hakuna uchaguzi wa aina yoyote uliofanyika katika Bunge hili na Bunge halikuhojiwa, haupo! Tutawaomba tupitie kwenye *Hansard*, haupo. Kwa sababu kama Bunge halikuhojiwa, Bunge litakuwa halikuamua. Halijaamua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa uamuzi unaweza kuwa ni *acclimation*, sauti au wa kura au kura za siri. Sioni sababu kwa nini mfike mahali mvutane. Katika jambo hili Kanuni za Uchaguzi hazikuweka wazi.

Sasa haijawahi kutokea tukapata wagombea walio sawa na idadi ya nafasi ili Bunge lifanye uamuzi wake. Kama mkataba unavyosema, lazima Bunge lifanye uamuzi, ukiachilia mbali uamuzi wa vyama, vinginevyo ungekuwa ni uamuzi wa vyama, ukija ndani basi Spika anasoma mnaondoka. Huo sio uamuzi. Kanuni ya 79 iko wazi kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashauri, wako wataalm wengi humu ndani. Tunafahamu mko wataalam, lakini kama tunataka kutumia utaalum, twende katika hili na sioni kwa nini tunakataa Bunge lisifanye uamuzi. Uamuzi wa kura ni uamuzi mmojawapo, uamuzi wa sauti ni uamuzi mmojawapo.

Mheshimiwa Spika, basi mchague ni uamuzi gani mnaotaka kuuchukua.

**MBUNGE FULANI:** Wa kura.

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH - MSIMAMIZI WA UCHAGUZI:** Sasa hata uamuzi wowote hamuutaki.

**WABUNGE FULANI:** Kura!

**DKT. THOMAS D. KASHILLILAH - MSIMAMIZI WA UCHAGUZI:** Haina shida.

**SPIKA:** Kwa hiyo, ni uamuzi wa kura eeh?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo!

**SPIKA:** Ahsante sana. Uamuzi wa kura; kura ya siri. Basi, Spika kwa kuzingatia ushauri aliopata anakubaliana na ninyi, utakuwa ni uamuzi wa kura; kura ya siri, kwa maana ya kwamba kwa wagombea hao utaweka kura ya tiki kumkubali au kura ya 'x' kumkataa.

Nini maana ya kura sasa? Mnaongea nini? Nini maana ya kura? (*Makofi*)

Sasa kwa hatua hii naomba *Returning Officer*, Maofisa wako waje na kura zigawanywe sasa. Nimefunga mjadala, gawa kura.

**MBUNGE FULANI:** Mawakala.

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH - MSIMAMIZI WA UCHAGUZI:** Naomba tugawe kura.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa ushauri tafadhali. Naomba unisikilize.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbowe, *with due respect*, nimeshafanya uamuzi sasa baada ya kuwasikiliza mno. Kwa hiyo, tugawe kura kama tulivyoshauriana, tupige kura.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Rudi kwenye Kamati ya Kanuni utafakari uamuzi wako bwana. Siyo sahihi.

*(Hapa Karatasi za Kura Ziligawiwa)*

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH - MSIMAMIZI WA UCHAGUZI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane kidogo. Mkipokea karatasi za kura, naomba niwape maelekezo.

Waheshimiwa Wabunge, kundi la wanawake unapigia kura nafasi mbili; wako wagombea wanne; kundi la Zanzibar nafasi mbili; kundi la kwanza A wanaume, unapigia kura moja na kundi B wanawake unapigia kura moja upande wa Zanzibar.

Vyama vya Upinzani, kundi C - kundi la kwanza CHADEMA, unapigia kura ya vema au kura ya hapana katika ki-box pembeni ya mgombea. Kundi la C chama cha CUF unapigia kura moja kwenye jina pembeni ya ki-box cha mgombea. Kundi B - Tanzania Bara unapigia kura mbili. Kwenye ki-box upande wa kulia kwenye picha ya mgombea.

Mheshimiwa Spika, nadhani maelekezo hayo yametosha. Baada ya kupiga kura naomba mkaenazo hapo hapo na mzifiche, tutakuja kuzichukua baada ya wote kuwa mmemaliza.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, hii inakuwa kura ya siri vipi tumekaa nazo huku?

*(Hapa Karatasi za Kura Ziligawiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, narudia tena kwenye makundi yale kama alivyosema Katibu. Kwenye wawili, tuchague wawili na kwenye mmoja, tuchague mmoja na kadhalika. Kwenye kundi lile la upinzani, hili ambalo limetuletea kelele nyingi hapa, kwenye *box* lile lile unaweka ama tiki ama 'x' pale pale kwa kila mgombea.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, sasa utaratibu gani wa kura ya siri watu wanaoneshana, wamefuata maelekezo ya chama? Wanafuata maelekezo ya chama wanapiga kura kwa kuoneshana. Hizo ndiyo kura za siri kwa mujibu wa Kanuni?

**MBUNGE FULANI:** Hizo kura siyo...

**SPIKA:** Naomba tumalize, ni zoezi la muda mfupi ili tuanze kukusanya kura.

*(Hapa Karatasi za Kura Ziligawiwa)*

**SPIKA:** Kuna Mbunge yeyote ambaye hajapata karatasi? Si yuko hapo mwenye karatasi? Msigawe karatasi tena mpaka nikwambie, wale wanaogawa karatasi. Kura moja peleka pale. Hapo ulishapeleka kura, unapeleka mbili mbili. Pale yule aliyenyoosha mkono pale ndiyo mpelekeeni kura. Ninyi Makatibu wangu mnanisikiliza au mmesimama kama miti hapo? Yule dada kule, mpe kura huyo.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, kura zinaoneshwa kwenye *screen*.

**SPIKA:** Kama kuna mwingine ambaye hajapata kura asimame. Makatibu msigawe kura tena, inatosha. Mkabebe masanduku ya kukusanya kura, mnanielewa, tokeni huko. Makatibu tokeni huko, njooni kati. Sitaki kumwona Katibu yeyote akizunguka huko tena, njooni katikati hapa mkachukue masanduku ya kura. Usigawe tena karatasi. Hivi hamnisikii ninachosema? Sitaki kumuona mtu na karatasi mkononi, rudisha huko. Kachukueni maboksi mkusanye kura. Fanyeni haraka.

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH - MSIMAMIZI WA UCHAGUZI:** Waheshimiwa Wabunge, kama mmemaliza kupiga kura tunaomba tukusanye karatasi za kura. Tunaomba mbaki na karatasi za kura mlipo, tutazifuata hapo hapo.

**SPIKA:** Vijana shikeni maboksi ya kura, inamisheni kwamba hayana chochote. Haya gawaneni kama Katibu atakavyowapanga ili muweze kukusanya kura.

**MBUNGE FULANI:** Hakikisha ni kura moja moja.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, hatujaambiwa idadi ya Wabunge ni wangapi.

**MBUNGE FULANI:** Haikuhusu.

**MBUNGE FULANI:** Wapo 600.

**MBUNGE FULANI:** Wewe unayesema, toka njiani.

**MBUNGE FULANI:** Shangazi yako.

**MBUNGE FULANI:** Si tumeambiwa hapa 333.

**MBUNGE FULANI:** Linamhusu shangazi yako Musukuma.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mtulie mahali penu ili kura zikusanywe.

**MBUNGE FULANI:** Wagombea wapeleke mawakala.

**MBUNGE FULANI:** Mawakala.

**SPIKA:** Naomba mtulie mahali penu ili kura zikusanywe.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Eeh, imeharibika. Huyu jamaa anaenda kuchukua karatasi nyingine, halafu utakuta ya kwake hajaweka.

**SPIKA:** Ambaye kura yake haijachukuliwa anyooshe juu kabisa ione kane. Wenye masanduku wahini kule ambako mnaoneshwa kura zenu. Katibu kama tayari njoo mbele. Naomba mliokuwa mnakusanya karatasi mje mbele...

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Spika, suala la utaratibu.

**SPIKA:** Mje mbele.

**MBUNGE FULANI:** Kura moja imeharibika huku.

**SPIKA:** Mje mbele. Aliyeharibu kura akabidhi iliyoharibika na apewe nyingine.

Waheshimiwa Wabunge, ambao mmekaa kwenye *corridor* nawaomba mtoke hapo. *Sergeant-at-Arms* nisaidie watoke hao wanaofanya kikao hapo mlangoni. Watoe wote hao. Sasa naomba *Sergeant* unilettee wagombea wote hapa ndani.

*(Hapa Wagombea Wote wa Bunge la Afrika Mashariki Wallingia Ndani ya Ukumbi wa Bunge)*

**SPIKA:** Viongozi wa kambi mnilettee majina, mmoja Kambi ya Upinzani na mmoja Chama Tawala ili wajiunge na watakaoteuliwa na wagombea ili waweze kwenda kule. Kila mgombea atateua mtu au yeye mwenyewe, lakini naomba ziada ya mmoja toka Kambi zote. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nasubiri majina ya wale wasimamizi wawili; mmoja Upinzani na mwingine Chama Tawala, lakini nataka kutoka kwa viongozi. Katibu wa CCM haraka haraka na Katibu wa huku au *Chief Whip* haraka naomba jina moja, mniandikie hapa. Wapeni watu wangu hicho kikatasi chenye jina. Niandikieni wapeni watu wangu wanilettee. Katibu aandikie haraka, nataka uhakika. Sitaki mtu atamke, nataka uhakika. Katibu nilettee. Watu wangu wapo hapa wachukue wanilettee, jina moja tafadhali.

Pamoja na vijana hawa ambao watashiriki kusaidia uhesabuji wa kura, kwa upande wa Upinzani ataenda Mheshimiwa Tundu Lissu na kwa upande wa Chama Tawala ataenda Mheshimiwa Abdallah Ulega. (*Makofi*)

Sasa kwa upande wa wagombea mna ruhusa ya kuteua mtu wa kwenda ama wewe mwenyewe, vyovyote utakavyoona inafaa. Naanza na... Naam!

**WABUNGE FULANI:** Waende wenyewe.

**SPIKA:** Mmekubaliana wote kwamba? Au kuna anayetaka kuweka mwakilishi? Ambaye haendi mwenyewe anataka kuweka mwakilishi, Mheshimiwa Kimbisa ndio umenyanyua mkono? Hamoud mbona wewe sio mgombea?

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Ni mwakilishi wa Kimbisa.

**MBUNGE FULANI:** Mwakilishi wa Kimbisa.

**SPIKA:** Aah, mwakilishi wa Kimbisa? *Okay*, nashukuru.

Sasa wale ambao mnaenda wenyewe hebu njooni upande huu wote. Yule ambaye haendi mwenyewe abakie hapo hapo ili tujue wawakilishi wake. Haya ninyi ambao hamwendi wenyewe, nipeni majina. Mheshimiwa Kimbisa tayari, Mheshimiwa Wenje, yuko Mheshimiwa Lema; Mheshimiwa Masha!

**NDG. LAWRENCE K. MASHA:** Mheshimiwa Waitara.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waitara. Haya, Mheshimiwa Waitara, Mheshimiwa Lema na Mheshimiwa Lissu naomba mjiunge na timu hapo.

Haya ninyi ambao hamtaki kwenda, basi mnaruhusiwa kurudi mlikotoka. Kwa nini usiende mwenyewe? Mheshimiwa Esther Midimu njoo kwa niaba ya Mheshimiwa Happiness Lugiko. Nadhani sasa mnaweza kufuatana na maboksi yenu mkaongozana nayo wote kwa pamoja

mkaenda kwenye chumba kilichoandaliwa. Mnaenda hivi, asiongezeke asiyehusika jamani. Nendeni na maboksi yenu. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa wakati wakihesabu kura na hii itachukua muda mrefu, nakupeni dakika chache, anayetaka kunyoosha miguu kidogo, anayetaka kupata kikombe cha chai, kwa hiyo, nendeni tu. Hatusitishi Bunge, na mimi mwenyewe niko hapa hapa, lakini anayetaka kunyoosha miguu, anayetaka kufanyaje; nadhani tutumie kama dakika 20 hivi halafu wote turudi hapa.

*(Hapa Karatasi za Kura Zilihesabiwa)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mnyika, Mwongozo.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, sasa hivi yamepita masaa takribani matatu, kwa hiyo, napenda kupata mwongozo wako kwa sababu naamini wewe unapata *update* ya kazi inayoendelea, tuendelee kusubiri kwa muda gani, hasa ukizingatia kwamba wengi wametoka hata ambao wapo kantini wengine wameshaondoka na kuna wengine wachache wamebaki nje, watu wanazidi kupungua. Tuendelee kusubiri kwa muda gani?

Mheshimiwa Spika, sasa hivi, bado robo saa siku mpya ianze. Naomba Mwongozo wako. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, msiwe na wasiwasi. Kazi hizi zinahitaji uvumilivu kwa vile ni lazima kutenda haki.

Kama mlivyoona, wagombea wote wameenda kule na kila mtu anataka utomaso, lazima kura aione kwa macho yake mwenyewe na kura hiyo lazima ipitishwe kwa idadi ya watu wote hao izungushwe mpaka ifike mtu wa mwisho. *(Kicheko)*



Kwa hiyo, ni kazi kidogo. Kwa taarifa nilizonazo, wameshavuka nusu kitambo. Kwa hiyo, msiwe na wasiwasi, hapa leo zege hakuna kulala mpaka kieleweke. Kama ni suala la *double* ya ile habari, linazungumzika. Kwa sababu kwa kweli leo mmefanya kazi. Kwa hiyo, tutaliangalia hilo kiofisi, maana haijapata kutokea. Kwa hiyo, tutahakikisha kuna *compensation* ya kutosha. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, waanze kurudi ndani, wanaweka sawa tu mahesabu, lakini uhesabuji *almost* umekamilika.

Ni dalili ya *commitment* kubwa sana mliyonayo kwa kazi hii na jinsi mnavyothamini kazi hii. Basi sasa nawaomba Waheshimiwa Wabunge mliopo mlangoni mkae kwenye viti vyenu, la sivyo mtoke nje. Ahsanteni sana.

Sasa nakuomba Katibu, *Returning Officer* uendelee na kutupatia matokeo ya zoezi lililoendelea pale ndani. Karibu Katibu.

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH – MSIMAMIZI WA UCHAGUZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba kwa mujibu wa Kanuni ya 13(3)(b) ya Kanuni za Bunge matokeo ya uchaguzi wa Bunge la Afrika Mashariki ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, idadi ya Wabunge Kikatiba waliopo ni 394; idadi ya Wabunge waliopo ni 390; idadi ya Wabunge waliopo na kupiga kura siku ya jana ya tarehe 4 Aprili, 2017 ilikuwa ni 334; idadi ya kura zilizoharibika ni moja. Naomba nisome matokeo.

Mheshimiwa Spika, Kundi A Wanawake; Fancy Haji Nkuhi alipata kura 197; Happiness Elias Lukigo alipata kura 196, Happiness Ngoti Mgalula kura 125 na Zainabu Rashid Mfaume Kawawa kura 137. Waliochaguliwa ni Fancy Haji Nkuhi na Happiness Elias Lukigo. (*Makofi/Vigelegele*)

**MBUNGE FULANI:** Wapi Martha Mlata. (*Makofi/Vigelegele*)

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH – MSIMAMIZI WA UCHAGUZI:** Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kundi B Tanzania Zanzibar; Abdullah Hasnuu Makame 254, Mohamed Yusuf Nuh kura 65, Maryam Ussi Yahya kura 195 na Rabia Hamid Mohamedi kura 142. Waliochaguliwa ni Dkt. Abdullah Hasnuu Makame na Maryam Ussi Yahya. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, kundi C; Vyama vya Upinzani walikuwa Wagombea wawili; Mheshimiwa Ezekiel Dibogo Wenje; kura za 'Ndiyo' ni 124 na kura za 'Hapana' ni 174. Lawrence Kego Masha, kura za 'Ndiyo' 126 na kura za 'Hapana 198.' Hakuna mshindi katika kundi hili.

Mheshimiwa Spika, upande wa Chama cha CUF kwenye kundi C, wagombea walikuwa wanne; Habib Mohamed Mnyaa kura 188, Sonia Juma Magogo kura sita, Twaha Issa Taslima kura 140. Mshindi ni Injiniya Habib Mohamed Mnyaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kundi D - Tanzania Bara; walioshiriki ni wagombea wanne; Adam Omari Kimbisa kura 266; Anamringi Issay Macha kura 23, Charles Makongoro Nyerere kura 81 na Dkt. Ngwaru Jumanne Maghembe kura 287. Waliochaguliwa ni Dkt. Ngwaru Jumanne Maghembe na Adam Omari Kimbisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo, wagombea waliochaguliwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki ni Wabunge saba. Nafasi mbili bado zipo wazi na nitaomba nisisome; Mheshimiwa Fancy Haji Nkuhi, Mheshimiwa Happiness Elias Lukigo, Mheshimiwa Dkt. Abdullah Hasnuu Makame, Mheshimiwa Maryam Ussi Yahya, Mheshimiwa Injiniya Habibu Mohmed Mnyaa, Mheshimiwa Dkt. Ngwaru Jumanne Maghembe na Mheshimiwa Adam Omari Kimbisa.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matokeo ya kazi yenu mliyoifanya na kama nilivyosema mwanzo, nawapongeza mno kwa vile ambavyo mmeonesha ushirikiano wa hali ya juu sana katika kazi za leo na mmeonesha uvumilivu mkubwa sana katika namna ambayo sikuitarajia hata kidogo. Kukaa hapa kwa masaa karibu saba na dakika kumi, masaa tisa sasa, saba au tisa, lakini ni muda mrefu sana, masaa tisa.

Kwa hiyo, tutaona kwamba katika matokeo yetu kama sikosei, Wabunge wa zamani waliorudi Bunge la Afrika Mashariki ni wawili tu na watano ni wanya. Haya ni mabadiliko makubwa sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, baada ya kufikia hatua hiyo, sasa naomba mniruhusu niahirishe shughuli za Bunge mpaka...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**SPIKA:** Katibu, kuna jambo lingine? Si hakuna! Naahirisha shughuli za Bunge hadi baadaye, leo saa 3.00 asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 7.13 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 5 Aprili, 2017 Saa Tatu Asubuhi)*